



EXTREMELY SMART

Wao Ima ni

WAEREVU MNO

AU

WAJINGA MNO

SALIM BOSS

MWEREVU MNO

Kshs. 900
Tshs. 17000
Others:
\$11 US

Maisha yako yanaweza kubadilika





Wao ima ni

**WAEREVU
MNO**

AU

**WAJINGA
MNO**



Salim Boss



Kimetolewa na
Extremely Smart

Tarjama ya kitabu cha Kiingereza
*"They are Either Extremely Smart or
Extremely Ignorant"* cha Salim Boss



Kimetolewa na **Extremely Smart**

ISBN: 978-9966-1628-1-6

www.extremelysmart.org



2012 Salim Omar Kenga

Haki ya Kunakili



Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kwa sehemu yoyote ya kitabu hiki kutengenezwa au kusambazwa kwa njia yoyote ile, ya kiteknolojia au kikawaida kama kutoa nakala bila ruhusa ya mwandishi, isipokuwa katika mazingira yafuatayo ambayo hapo utapata ruhusa hiyo.

Kwa Kutoa Nakala ya Kitabu

Kusambaza na kutoa nakala nyengine kwa njia nyengine ambazo kwa hali yoyote hakutaongezwa wala kupunguzwa kitu mathalan kichwa cha kitabu, jina la mtunzi, haki za kunakili hapo juu kuainishwa, anuani ya mtunzi, na maelezo haya yahusuyo kutoa nakala yasiondolewe kama vile kitabu halisi kilivyokuwa, **na iwe kwa matumizi yasiyo ya kibiashara** basi kutaruhusiwa tena **bila fidia** yoyote. Kwa kuhakikisha usahihi wa nakala ya kitabu, na kupata toleo jipya la kitabu, ni vyema ukawasiliana na mwandishi kupata matoleo yaliyokuwa tayari. **Kuwasiliana na mwandishi, tazama ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki.** Na *Tovuti* yake ni:

www.extremelysmart.org

Kimetarjumiwa na **Mussa Moses**





Toleo la *King James Version* (linalojulikana kwa jina *Biblia* kwa lugha ya Kiswahili) ndilo lililotumika kunukuu maandiko yote ya Biblia ispokua yale yaliotajwa kunukuliwa kutoka kwenegineko. Vifungu vya maneno vinukuliwavyo kutoka katika maandiko matakatifu vitakuwa katika muonekano ufuatao:

Biblia: **Rangi ya Samawi**

Qur'an: **Rangi ya zambarau**

Hadithi za Mtume Muhammad: **Kijani**



***“Walo hatari kuliko wote
ni wale wajinga”***

~ Henry Ward Beecher* (1813- 1887)

* Alikuwa kasisi kanisani na mwanaharakati katika jamii, alikuwa mhubiri mkubwa kuliko wote Marekani kwa wakati huo.


*“ Najikinga kwa
Mwenyezi Mungu
nisiwe miongoni mwa
wajinga.”**

~ Musa (Mtume kwa Wana wa Israeli)

*Qur'an 2:67

*“Enyi wajinga,
hata lini mtapenda ujinga?
Na wenye dharau kupenda
dharau yao, Na wapumbavu
kuchukia maarifa? Geukeni kwa
ajili ya maonyo yangu; Tazama,
nitawamwagia roho yangu,
Na kuwajulisheni maneno
yangu.”*

[Mithali 1:22-23]



***“Maisha yalianza upya
kwa kuwa nilifungua
kurasa (nikasoma)”***

~ Alberto Manguel

FAHIRISI

Dibaji.....xiii

Nukta Ya Msingi.....xx

SEHEMU YA 1

WAONGOFU.....1

1.1

Dini Inayokuwa Kwa Kasi Kuliko Zote.....2

Akili Yenye Kufikiri Kwa Kasi.....3

Hawa Ima ni Waerevu au Wajinga.....7

Kuyakataa Mabaya na Kuyachagua Mema.....11

Takwimu Zitaongea kwa Sauti Zaidi.....14

Uislam Unakuwa kwa Watu Kusilimu.....19

Nzi Bilioni Moja Hawawezaji Kuwa Makosani.....24

1.2

Watu Waerevu na Machaguo Sahihi.....26

Baadhi ya Watu Waerevu Waliofanya Maamuzi Sahihi.....27

Murad Wilfried Hofmann.....27

Yvonne Ridley.....35

Jeffrey Lang.....43

Khadijah 'Sue' Watson.....49

Cat Stevens.....51

Jemima Goldsmith.....59

Malcolm X.....62

Dkt. Fidelma A. O'Leary.....82

Yusuf Estes.....84

Sara Bokker.....94

Subeib Webb.....98

Ingrid Mattson.....104

<i>Kareem Abdul-Jabbar</i>	110
<i>Susanne Osthoff</i>	123
<i>Dkt. Timothy J. Winter</i>	128
<i>Rosalyn Rushbrook</i>	138
<i>Muhammad Ali</i>	147
<i>Dkt. Lisa Zaynab Killinger</i>	160
<i>Dkt. Jerald Frederick Dirks</i>	164
<i>Aminah Assilmi</i>	174
<i>Rabbi Yusuf Cohen</i>	179
<i>Mary Fallot</i>	186
<i>Dkt. Gary Miller</i>	187
<i>Kristiane Backer</i>	193
<i>A.R. Rahman</i>	200
<i>Sarah Joseph</i>	205
<i>Musa Cerantonio</i>	210
<i>Balqis Chelang'at Chepkwony</i>	222
<i>Michael Wolfe</i>	237
<i>Elizabeth</i>	246
<i>Lord Headley al-Farooq</i>	250
<i>Dkt. Kari Ann Owen (Penomee)</i>	257
<i>Jermaine Jackson</i>	261
<i>Nicole Aeschleman</i>	269
<i>Loon, The former Bad Boy artist</i>	274
<i>Lim Bee Ping</i>	284
<i>Keith Ellison</i>	285
<i>Susan Carland</i>	298

1.3

Kisa Nikipendacho Zaidi.....305

<i>Kwanini Kive Kisa Nikipendacho Zaidi</i>	306
---	-----

1.4

Yanayosemwa na Wengine Waliosilimu...329

<i>Maono ya Wengine Waliosilimu.....</i>	<i>330</i>
<i>Abdul Azim (Greogor Shepard).....</i>	<i>330</i>
<i>Abdussalam Sipes (Clinto Sipes).....</i>	<i>331</i>
<i>Ahmed Holt.....</i>	<i>331</i>
<i>Alfonse Etienne Denier.....</i>	<i>332</i>
<i>Ali Selman Benoist.....</i>	<i>332</i>
<i>Ali (Vyacheslav) Polosin.....</i>	<i>333</i>
<i>Aminah Vanderdrift.....</i>	<i>333</i>
<i>Angela (Germany Lady).....</i>	<i>333</i>
<i>Bogdan Dopanski.....</i>	<i>334</i>
<i>Busbra Finch.....</i>	<i>334</i>
<i>Kapteni Yahya M.A. Ondigo.....</i>	<i>335</i>
<i>Kanali Donald S. Rockwell.....</i>	<i>337</i>
<i>Dkt. Grenier.....</i>	<i>337</i>
<i>Dkt. Hamid Marcus.....</i>	<i>338</i>
<i>Erin Saumaya Fannoun.....</i>	<i>338</i>
<i>Haj Dkt. Abdul-Karim Satio.....</i>	<i>339</i>
<i>Herbert Hobohm (Aman Hobohm).....</i>	<i>339</i>
<i>Ibrahim Khalil (Philobus).....</i>	<i>340</i>
<i>Izzat Heath.....</i>	<i>340</i>
<i>Jennifer Harrell.....</i>	<i>340</i>
<i>Jim Hacking.....</i>	<i>341</i>
<i>Juba Abdullah Ali.....</i>	<i>341</i>
<i>Karen Meek.....</i>	<i>341</i>
<i>Karen Courtenay.....</i>	<i>342</i>
<i>Karima Slack Razi.....</i>	<i>342</i>
<i>Khadija Evans.....</i>	<i>343</i>
<i>Lawrence E. Browne.....</i>	<i>343</i>
<i>Leopold Weiss (Muhammad Asad).....</i>	<i>344</i>
<i>Leyla Chepchirchir.....</i>	<i>344</i>
<i>Lisa.....</i>	<i>345</i>
<i>Lord Douglas Hamilton.....</i>	<i>346</i>
<i>Maariyah.....</i>	<i>346</i>
<i>Margaret Marcus (Maryam Jamilah).....</i>	<i>347</i>
<i>Marmaduke Pickethall.....</i>	<i>348</i>

<i>Marshila Michelangelo</i>	349
<i>Maurice Bucaille</i>	349
<i>Monica Nur Sammour-Wüst</i>	350
<i>Neil Sharp</i>	351
<i>Nicole Banks</i>	351
<i>Noora Brown</i>	352
<i>Nouria</i>	352
<i>Nuh Brecheen</i>	353
<i>Professor Haroon Mustapha Lion</i>	353
<i>Saifuddin Dirk Walter Mosig, U. S.A.</i>	354
<i>Sarah Jacobs</i>	354
<i>Sir Archibald Hamilton (5th Baronet)</i>	355
<i>Tejatat Tejasen</i>	356
<i>Ummu Travis</i>	356
<i>Vengatachalam Adiyar</i>	357
<i>Yahya Donald W. Flood</i>	357
<i>Zabrah Riddle</i>	358

1.5

Wengine Mashuhuri Waliojiunga na Uislamu.359

<i>Watu Wengine Zaidi Walioifuata Uislamu</i>	360
---	-----

SEHEMU YA 2**JE UISLAMU UTATAWALA?.....384**

<i>Idadi Kubwa, Maana Kubwa</i>	386
<i>Je Hawajaona Bado Kama Uislamu Unaelekea Kutawala?</i> ..	404
<i>Kinachowapunguza</i>	408
<i>Dini ya Wote</i>	415
<i>Kila Mtu Anataka Kutawala, Yupi Tanayewafikiana Naye?</i> ..	449
<i>Kama Uislamu ni Tishio kuwa Maisha Yetu, je! Yatupasa Kuipiga Vita?</i> ..	473
<i>Jua Linachomoza Magharibi</i>	484

SEHEMU YA 3**YESU ALIKUWA NI NJIA, UKWELI NA UZIMA.....487**

Mwenyezi Mungu Anafungua Vifua Vyao Kuuelekea Uislamu.489
Kama jina langu ni Rocky (jabali) la baba yangu ni Stone (jawe), na Mahogany
(mkanga'zi) lime jina la ukoo, je yanipasa kubadilisha majina?.....508

SEHEMU YA 4**KAMA TUNGALIKUWA NA AKILI..513**

<i>Ujasiri wa Kuwa Mjinga.....</i>	<i>515</i>
<i>Lengo la Maisha.....</i>	<i>522</i>
<i>Kwanini Mungu Atutelekeze?.....</i>	<i>534</i>
<i>Uteremsbo Sahibi.....</i>	<i>542</i>
<i>Imani ya Upofu.....</i>	<i>548</i>
<i>Kutumia Ubongo Sasa Kutafiti Maandiko/ Dini.....</i>	<i>552</i>
<i>Ugonjwa wa "Nafikiri".....</i>	<i>565</i>
<i>Kutoifuata Dini ya Kweli Baada ya Kuigundua.....</i>	<i>567</i>
<i>Kuendelea kwa Uislam.....</i>	<i>569</i>
<i>Dini ni Ngumu.....</i>	<i>571</i>
<i>Waislamu Wasiofuata Uislamu Kikamilifu.....</i>	<i>582</i>
<i>Tumaini la Mabadiliko.....</i>	<i>585</i>
<i>Kufikiria Yatakayojiri kwa Umakini.....</i>	<i>588</i>
<i>Adhabu Ndogo Zaidi Motoni.....</i>	<i>592</i>
<i>Ujinga Uliothibitishwa.....</i>	<i>596</i>

Kwa Ufupi (Summary).....601**Kwa Usomaji na Usaidizi wa Ziada.....602****Picha za Vitabu Vilivyoshauriwa.....632****Bibliografia.....640****Rejea za Vyombo vya Habari.....646****Kwa Wasomaji Wangu.....648**



Dibaji

Wasiokuwa Waislam wengi kama Mayahudi, Manaswara, wafuasi wa dini za Kihindi, Mabudha, Wapagani na wengineo hawajaelewa au kwa upande mwengine hawajajaribu kwa makusudi kuelewa madhumuni, imani, itikadi na dalili za makundi mengine ya dini. Hii inawanyima ufahamu wa ukweli kama upo katika dini nyengine yoyote. Huu ndio uhalisia, kama ilivyoelezwa na mwanazuoni mkubwa wa zamani katika jangwa la Arabia, Ali ibn Abi Talib, ambae alisema, “Kama mtu ni mjinga au hana ufahamu wa jambo fulani, ni rahisi kwake kulipinga”. Na ni huzuni iliyoje watu kwa makusudi wanakosa ufahamu wa jambo ambalo ni muhimu kwa wao wenyewe. Na siku zote, watu wasiojua kitu hulalamika kwa kubwata kwa sauti kubwa dhidi ya wale ambao inawezekana wanatembea katika njia nyoofu. Kama yule mwanamke mpumbavu katika Mithali 9:13-15, “*Mwanamke mpumbavu hupiga kelele, Ni mjinga, hajui kitu. Hukaa mlangoni pa nyumba yake, Juu ya kiti mahali pa mjini palipoinuka. Apate kuwaita wapitao njiani, Waendao moja kwa moja katika njia zao.*”. Mfano kuonesha jinsi gani watu hawana ufahamu na imani yao wenyewe, achilia mbali na wengine ni pale George Gallup, kiongozi wa utafiti wa masuala ya kidini anaelezea kuwa Marekani ni taifa la watu wasiojua Biblia. Katika pembuzi zake Gallup, aligundua kuwa ni chini ya nusu ya Wamarekani wanaweza kukitaja kitabu cha kwanza katika Biblia, yaani Mwanzo, asilimia sitini (60%) wameshindwa kutaja nusu tu ya amri kumi (10) alizogaiwa Mussa, na wengine nusu wanafikiri Nuhu alimuoa Joan¹. Pia ungependa kusikia mfano sambamba na huo kutoka kwa Dkt. Bart Ehrman ambaye ni mtunukiwa wa tuzo la Profesa wa Teolojia wa Taasisi ya James A. Gray ambaye anafundisha masomo ya dini katika Chuo Kikuu cha North Carolina, huko Chapel Hill, na pia ana mamlaka ya juu (msomi mtegemewa) katika Biblia na maisha ya Yesu. Kila mwaka Dkt. Ehrman huwauliza wanafunzi wa shahada ya mwanzo kuhusu

1. “The Bible v the Koran, the battle of books.” *The Economist* 22 Dec. 2007: p.60.

mouno wao katika Biblia, na cha kushangaza huwa anapata majibu yanayoshabihiana. Anasema,

“Siku ya kwanza darasani katika wanafunzi zaidi ya mia tatu, huwa nawauliza: “Nani kati yenu anaamini kidhati kuwa Biblia ni neno la kweli la Mungu?” Looh! Karibu kila mtu huwa ananyoosha mkono. Nauliza tena, “Nani kati yenu amesoma kitabu kimoja au zaidi katika vitabu vya Harry Potter?” Looh! Darasa zima huwa linanyoosha mikono. Cha kushangaza huwa pale nikiwauliza, “Nani kati yenu amemaliza kusoma Biblia nzima.” Mikono inakuwa ya kuhesabika, ni wanafunzi wachache tu wanyoosha mikono.”²

Kwa mwenendo huu, tuna uhakika gani kama bado hatuna ufahamu wa imani ya Kiislamu? Na kabla ya kuendelea na kitabu, ni muhimu kujikumbusha maana ya neno “mjinga”. Katika *Kamusi ya Merriam-Webster* inatafsiri neno mjinga (ignorant) kama (1) ukosefu wa maarifa au uelewa wa jambo fulani (2) kutokana au kuonesha ukosefu wa maarifa au akili. Na tukitumia *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Dar-es-Salaam, tutaona kuwa neno “mjinga” lina maana ya “mtu asiyejua kitu au jambo fulani; fala, jura, gulagula, bozi, mpumbavu, juha.”³ Kitabu hiki kimeendelea kuwaanika watu ambao wanapoteza maisha yao kwa kujipa ujinga wa makusudi katika masuala ya msingi na yanayotakiwa kujaliwa katika maisha. Craig R. Smith ni mtunzi, mtangazaji na mkurugenzi wa shirika la kibiashara la Swiss Amerika (Swiss America Trading Corporation), kampuni ya uwekezaji iliyojikita katika utengenezaji wa sarafu za dhahabu na za fedha za kimarekani. Anasema, “mtu kuwa mjinga ni mtu kiuwazi kabisa kupinga au kudharau ukweli au uhalisia”. Kama alivyosema Craig Smith, “Kudharau au kutojali ukweli au uhalisia uliowekwa wazi unatupa watu

2. Ehrman, Bart D. *Jesus, Interrupted*. Kindle Edition. HarperCollins e-books, 2009.p.226.

3. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo La Pili. Nairobi: Oxford University Press, 2004. p. 249.

wajinga...”⁴ vilevile katika kitabu hiki, watu wajinga watajijua kama wataendelea kufanya jitihada ya kudharau ukweli wowote unaopita mbele yao. Inashangaza wakati asiye Muislam akiusoma Uislam na kuamua kubadili dini, waliobaki wanamchukulia kama kondoo aliyepotea, msaliti, mjinga anayefata udanganyifu, mleta aibu, aliyechanganyikiwa, mtu wa kipekee mwenye tabia za ajabu ajabu, karogwa, mwendazimu, mfurahia kubezwa, mdhaifu wa fikra, anaemini kila kitu kipumbavu, na ni mjinga mno - hayo ni machache tu. Sasa, nani ni mjinga na nani ni mwerevu? Jibu litawekwa wazi na kitabu. Will Rogers, anaelezea katika msingi ufuatao: “Mtu mjinga ni yule ambae hajui kipi ulichokigundua.” Kujiepusha na kunasibishwa na wajinga, acha tujijuze katika yapi hawa waliobadilika wamekigundua.

Kutokana na watu wa dunia kugawanywa, wajinga au waerevu, kitabu kinaondoa ukungu na kinampa msomaji uono mzuri wa kugundua na kutenganisha wajinga na waerevu. Kitabu kitatusaidia kubainisha na kupambanua yaliyojiri kwa hawa waliobadilika, ili itusaidie kuwajua kinaga ubaga kama ni waerevu kweli au wajinga. Nasisitiza, hiki sio kitabu cha kukwepa kueleza nukta za msingi na wala sio kitabu ambacho chepe litaitwa kijiko kikubwa (au reki kuitwa uma mkubwa). Na bila shaka kitabu hiki kipo kwa madhumuni ya kuamsha ufikiri wa jirani yako katika masuala mazima ya imani. Kama ni kweli kama wengine wanavyodai, kuwa waliokubali Uislam wamechukua uamuzi wa kijinga, tukumbuke pale *Rikodi za Dunia za Gines (Guinness World Records)* za 2003 zilivyosema, “Katika kipindi cha 1990 mpaka mwaka 2000, takriban watu milioni kumi na mbili unusu (12.5) wameingia katika Uislam zaidi ya wale walioingia katika Ukristo”⁵, pia pale gazeti la *St. Petersburg Times* lilivyoandika, “Kila mwaka, kiasi cha watu wapatao elfu ishirini (20,000) wanaingia katika Uislam katika taifa la Marekani...”⁶, na kumbuka Samuel Huntington

4. Smith, Craig R. “America: An ignorant nation.” [wnd.com](http://www.wnd.com/index.php?pageId=94749) 13April 2009. <<http://www.wnd.com/index.php?pageId=94749>> retrieved 3/01/2010

5. *Guinness World Records* 2003. p. 102.

6. Wiener, Jocelyn (Times Staff Writer). “Young, Female and Muslim.” *St. Petersburg Times* 7 Oct. 2002.

alivyotabiri kwamba ifikapo mwisho wa karne ya Ishirini na moja, idadi ya Waislam itaipiku ile ya Wakristo⁷, kutokana na mifano hii yapasa tukubaliane kuwa dunia inaburuzika kuelekea katika wajinga wengi.

Kwa kuwa ukweli sio milki ya yeyote, kitabu kitachomoa kutoka katika vyanzo tofauti, kama katika Biblia, Qur'an, Hadithi za Mtume Muhammad, wanafalsafa wa mashariki na magharibi, wasio weledi, na hata kutoka kwa sheitan kwani sheitan wakati mwengine pia husema ukweli. Muhammad, mtume wa Waislam alinukuliwa kukubali maneno ya shetan pale aliposema, “**Katika hilo, sheitan ameongea ukweli japokuwa huwa ni Muongo siku zote....**”⁸ na katika maneno ya Shekspia (Shakespeare), “Shetani anaweza nukuu andiko...”⁹ Kimsingi, chochote kitachonenwa na kitabu hiki ni kile kinachoendana na ukweli bila kujali nani aliyesema. Tutaendana na kanuni ya Malcolm X: “Mimi nasimamia ukweli, haijalishi anausema nani”

Katika kitabu kilichotolewa kwa lugha ya Kiingereza (***They are Either Extremely Smart or Extremely Ignorant***), maandiko ya Kibiblia yametolewa kutoka katika *New King James Version* (NKJV) kutokana na umaarufu na kukubalika kwake na wengi, na pia kutoka *The New Revised Standard Version* (NRSV) kwa sababu lina ridhaa ya kukubalika kwa mapana kabisa kati ya tafsiri zote za Biblia. Lakini katika kufasiri hiki kitabu, tarjama ya Biblia iliyotumiwa zaidi ni ya *King James Version* inayojulikana kwa jina *Biblia* iliyotolewa na Chama Cha Biblia Cha Tanzania na Kenya (The Bible of Societies of Kenya, Tanzania). Hii ni kutokana na kutokuwepo na tarjama ya Kiswahili ya hizo Biblia zilizotumika katika kitabu cha Kiingereza.

7. Huntington, Samuel P. *The Clash of Civilizations and the Remaking of World Order*. New York: Simon & Schuster, 1996. pp. 65-66.

8. Bukhari, Vol. 4, bk.54, No. 495.

9. Shakespeare, William. *The Merchant of Venice*. Act I, Scene 3.

Profesa A. Guillaume anakiri kuwa, “Qur’an ni moja kati ya hazina za zamani za dunia ambayo haiwezi kufasiriwa bila ya mpotevu mkubwa.”¹⁰ Muono kama huo ukaletwa na baadhi ya wafasiri wa Qur’an, kama vile Marmaduke Pickthall na Profesa A.J. Arberry, ambae alisema: “Katika kuchagua kuiita kazi ya sasa *The Qur’an Interpreted*’, nimekiri umuhimu wa msemo wa Waislam wengi ambao hata Pickthall anautambua, kwamba Qur’an haitafsiriki.”¹¹ Kutokana na hivyo, nukuu za Qur’an katika kitabu hiki (kilichotolewa kwa lugha ya Kiingereza) zilichukuliwa kutoka kwa tafsiri ya Abdullah Yusuf (*The Holy Qur’an: Translation and Commentary*), na tafsiri ya Saheeh International, muungano wa Muhammad Al-hilal na Muhammad Khan (*The Noble Qur’an*). Lakini katika toleo hili la Kiswahili, Tafsiri ya Qur’an iliyotumika ni ile *Tarjama ya Al-Muntakhab Katika Tafsiri ya Qur’ani Tukufu* iliyotarjimiwa na Sheikh Ali Muhsin Al-Barwani. Pia tumetumia ile iliyofasiriwa na marehemu Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy inayoitwa *Qurani Takatifu*. Sababu ya kutumia tafsiri nyingi kwa pamoja ni kutokana na ukweli kwamba Kiarabu sio lugha nyepesi kutafsirika bila utata wowote. Hivyo basi, tumaini letu ni kuwa kwa kutumia tafsiri nyingi kwa pamoja tutajaribu kufikisha tafsiri halisia ya mwanzo.

Kitabu hiki kimepangiliwa katika mtindo ambao utakuwa rahisi kusomeka, kuburudisha, na kumeng’enywa bila matatizo. Hivyo

► Vifungu vya maneno yote yaliyo katika ulalo, vinaonesha msisitizo wa mtunzi. Pia vifungu vya maneno vinavyooneshwa kwa rangi ya manjano pia vinaonesha msisitizo wa mtunzi. Kwa mfano “...hakutaka kuiuza akili yake.”

► Vifungu vya maneno vinukuliwavyo kutoka katika vitabu vitakuwa katika muonekano ufuatao:

Biblia: **Rangi ya Samawi**

Qur’an: **Rangi ya zambarau**

10. Guillaume, Alfred. *Islam*. Penguin Books, 1990. pp. 73-74.

11. Arberry, A. J. *The Koran Interpreted*. A Touchstone book: Simon & Schuster, 1996. Preface, p. 24.

Hadithi za Mtume Muhammad: **Kijani**

► Popote uonapo herufi Q kama (Q 11:46), inafupisha Qur'an Sura ya 11 aya ya 46.

► Nukuu zioneshazo ukweli wa kisomi zitawekwa kama zilivyo, japokuwa nukuu zenye msukumo na motisha hazitakuwa na ulazima wa kuwekwa. Namaanisha zile za kawaida, zinazoeleweka ambazo hazina haja ya kuelezwa kwa mfano “ujinga ni mzizi wa maovu yote”.

► Maelezo muhimu ya ziada na marejeo mtambuko (cross-references) huelezwa chini ya kila kurasa.

► Picha zimewekwa kwa kuwa picha moja ina thamani ya maneno elfu moja katika kuelekeza.

► Kuepuka madai ya kuweka watu au visa vya uongo, rejea za visa hivyo zimewekwa katika kila mwisho wa habari yake. Hiki ni kitabu kinachokupa fursa ya kuhakikisha mwenyewe.

Popote watu mashuhuri na wakubwa katika historia kama Yesu na Muhammad wanapotajwa, lazima wapewe heshima zao. Katika kumtaja Yesu, Waislam huwa wanaambatanisha na “Amani iwe nae” na wanapomtaja Muhammad, Waislam huwa wanaomba “Rehema na Amani ziwe juu yake”. Hata hivyo, mtindo huo hautatumika sio kwa kuwa hatutaki kuonesha heshima kwao bali ni kujaribu kuonesha kujali kwetu watu wenye imani zisizokuwa za Kiislamu. Hivyo tutasema hapa kabisa, “Amani iwe juu yake yule afataye muongozo wa haki na ukweli”.

Kitabu hiki ni tangazo la kisomi la kitendo hiki kikubwa cha watu kuingia katika Uislam, wengine wanaweza dhani ni kitabu cha kuhamasisha na kusilimisha watu lakini ukweli ni kuwa hayo waliyofanya ni uamuzi na hukumu yao. Kitabu hiki kimejazwa ukweli mwingi sana na hoja zisizopingika na wala sio kauli au maelezo ya kihisia na jazbu tu yaliyoko mbali na ukweli na uhakika. Kwa yeyote ambaye anataka kupuuza au kupinga ukweli na hoja zilizojaa katika hiki kitabu kwa kuleta hoja na “ukweli” tofauti, kwa moyo mkunjufu namwambia “.....Leteni hoja zenu kama

nyinyi ni wasema kweli.” [Q 27:64] Vile vile naweza kukualika sasa kwa kukwambia, “**Njoni, basi, tuhojiane....**” [Isaya 1:18, Tafsiri ya Biblia iitwayo *Habari Njema (Good News)*]. Kitabu hiki ni wito kwa wakazi wa sayari hii ili wapange upya mipango yao kwa jinsi gani watanufaika, ima kiuchumi au vinginevyo na maisha ya karibuni kuja yenye Waislam wengi zaidi. Kama Rais Obama alivyosema katika hotuba yake ya kuapishwa ya 2009: “Kwa Waislamu wote duniani, tunahitaji maisha mapya yatakayotokana na kuheshimiana na maslahi yanayoridhiwa pande zote.”

Nairobi,
Novemba, 2012.

Salim Omar Kenga





NUKTA YA MSINGI

Vitabu rejea, tovuti, video na venginevyo vimetumika humu kwa lengo la kuthibitisha tu habari za waliosilimu na kuenea kwa Uislamu. Mafundisho yoyote yaliyoko katika rejea hizo yaendayo kinyume na mafundisho ya Uislam hayatahusika na mtunzi wa kitabu hiki. Kupotoka kokote kutakoonekana na walioainishwa humu hakuhusiki na Uislam. Uislam utabaki kuwa kweli na wa haki siku zote. “Anaye ongoka basi anaongoka kwa ajili ya nafsi yake. Na anaye potea basi anapotea kwa khasara yake mwenyewe. Wala habebi mbebaji mzigo wa mwengine.” [Q 17:15]. Kama ilivyo, “Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa; mwana hatachukua uovu wa baba yake, wala baba hatachukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake.” [Ezekieli 18:20] Acha kila mtu na aubebe mzigo wake.



SEHEMU YA KWANZA

WAONGOFU

(Waliosilimu)

Sehemu ya 1.1

Dini Inayokuwa kwa Kasi Kuliko Zote



Ni tabia ya uyoga kuchipukia
kwa kasi sana



“...Hivyo nikauliza, wafuasi wake huwa wanaongezeka au wanapungua. Ukanijibu kuwa ni kweli wafuasi wake wanaongezeka. Nikakuuliza tena kama kuna yeyote ambaye baada ya kuongoka kwa kuingia katika dini hii akawa hajaridhishwa na kuamua kuikana dini hii; jibu lako likawa hasi. Hakika, hii pia ni dalili ya imani ya kweli kwani baraka zake zinapomwiingia mtu na kuchanganyika katika moyo kikamilifu, hakuna anayekuja kutoridhishwa nayo....”¹

~Heraclius, Kaizari wa Kirumi

Akili Yenye Kufikiri Kwa Kasi

Akili yenye kufikiri huwa inashtushwa na taarifa kama “Waislamu ndio kundi linalokuwa kwa kasi zaidi duniani....”² ambayo ilichapishwa na gazeti lililoenea na kusomwa na wengi Marekani, *USA Today*. Akili yenye kufikiri itashuhudia Hillary Rodham Clinton akisema, “Uislam ndio dini inayoenea kwa kasi zaidi Marekani, ni mwongozo na nguzo ya uimara kwa wengi wa watu wetu....”³ na kushughulishwa. Na baada ya kusikia kutoka katika Shirikisho la Habari la Uingereza (BBC) ambapo Mike Wooldridge akiripoti kuwa, “Uislam ndio imani inayokuwa kwa kasi zaidi....”⁴, bila shaka kwa mtu mwerevu na mwenye kutumia akili yake ipasavyo atajenga wazo akilini mwake kuwa “Huenda dini hii ikawa ndio dini ya kweli”. Kisha akisoma *The Junior Encyclopedia of Canada* ilotanabaisha:

1. Baada ya kumdadisi Abu Sufyan kuhusu wafuasi wa Muhammad, Heraclius alitoa maoni hayo. [Angalia Bukhari Vol.4, Bk. 52, No. 191.]
2. Kenny, Timothy. “Elsewhere in the World.” *USA Today* Final Edition 17 Feb. 1989: p.4A.
3. Stammer, Larry B. (Times Religion Writer). “First Lady Breaks Ground With Muslims.” *Los Angeles Times* Home Edition, Metro Section, Part B, 31 May 1996: p.3.
4. Wooldridge, Mike. “Islam: Faith under fire.” [news.bbc.co.uk](http://news.bbc.co.uk/1/hi/world/americas/1544071.stm) 14 Sept. 2001. 11:17 GMT 12:17 UK. <<http://news.bbc.co.uk/1/hi/world/americas/1544071.stm>>

“Uislam ndio imani inayokua kwa kasi zaidi ulimwenguni”⁵ atatafakari, akitumia akili zake vizuri na kulazimika kuweka chuki zake kando na kuutazama ukweli, hata kudiriki kuuona Uislam kuwa ndio badiliko la msingi, muhimu na la kweli. “...Sheria ya Muhammad imekutana na mapokezi yasiyofanana nayo kabisa hapa duniani....”⁶ hii iliandikwa na George Sale, mmoja kati ya wa mwanzo kuitafsiri Qur’an kwa lugha ya Kiingereza, aliyejitunuku shahada ya mpingaji mkubwa wa Muhammad na mchukiaji wa dini ya Kiislam. Kuongezea hilo, “Hakuna dini nyengine ieneayo kwa kasi zaidi kuliko Uislam”⁷ iliyoandikwa na James Michener, mwandishi mashuhuri na mshindi wa zawadi ya waandishi bora wa Pulitzer. Mtu mwenye chuki na dhara ya hali ya juu anaweza kusikia sauti ndogo kichwani mwake ikinong’ona, “ Wewe! Ni bora ukubali walau mara moja tu kuwa kuna jambo kubwa katika Uislam.” Na pale jarida la *The Economist* wanapoitanabaisha dunia kuwa “Wengi kati ya wasomi wa Kikristo wanakubali kuwa Uislam utaupita Ukristo kama dini yenye wafuasi wengi na inayoenea kwa kasi kabla ya mwaka 2050.”⁸ inabidi watu waendele kuwa wakimya wakipea mazingatio na kutafakari usukani.

Kama hiyo haitoshi, kipande cha habari kilichotolewa kutoka katika jarida la *National Geography* la mwezi wa kwanza (January) 2002 lilielezea kuwa “Khumusi (moja ya tano) ya wannadam sasa wanafata Uislam, dini inayokuwa kwa kasi zaidi japokuwa ndio dini inayoeleweka vibaya kuliko zote duniani.”⁹

Tarehe 17 Julai 1997, mkurugenzi wa *Christian Futures Network*, John Gary baada ya kupokea zawadi yake katika World Future Society (tamasha linalojadili jamii za kesho za kidunia), alisikika akiongelea “Matukio kumi ya dunia yahusuyo dini” na katika tukio la tatu alitamka “Miongoni mwa dini za hapa ulimwenguni,

5. *The Junior Encyclopedia of Canada*. Hurting Publishers, 1990. Vol. 2, p.396.

6. Sale, George. Preface. *The Koran*. London: C. Ackers, 1734. A2.

7. Michener, James A. “Islam: The Misunderstood Religion.” *Reader’s Digest* American Edition. May 1955: p. 73.

8. “The Bible v the Koran, the battle of books.” *The Economist* 22 Dec. 2007: p.62.

9. Belt, Don. “The World of Islam.” *National Geographic* Jan. 2002.

Uislam unashika nafasi ya juu kwa ukuaji wa kasi....katika takwimu za kipindi cha baadae, haitashangaza kuona Uislam ukiupiku Ukristo kwa kuwa na idada ya wafuasi wengi zaidi.”¹⁰ Hiyo ni tabiri moja, lakini kwa akili isiyo na upendeleo wowote utauona Uislam kupitia lenzi yenye kuheshimika baada ya kusoma tabiri nyengine ya msomi mashuhuri Samuel Huntington akitabiri kuwa:

“Asilimia ya Wakristo duniani...utafikia takriban asilimia 25 ya watu wote duniani kabla ya mwaka 2025....Japokuwa Waislam wataendelea kuongezeka kwa kasi ya ajabu, kufikia asilimia 20 ya watu kabla mwanzo mwa karne ya 21 kufunika idadi ya Wakristo miaka kadhaa baadae na hata uwezekano wa kufikisha asilimia 30 ya watu kabla ya mwaka 2025.”¹¹

Wakati *Kitabu cha Maarifa cha Guinness (Guinness Book of Knowledge)* kilikiri kuwa Uislam ndio dini inayokuwa na kuenea kwa kasi zaidi duniani¹², kwa yeyote muungwana, mpenda ukweli na mwenye fikra za haraka atakubali kuwa Uislam utakuja kutawala mambo yote ya kilimwengu. Lakini mwishoni, *Guinness World Records 2003*, kitabu chenye mamlaka na chenye mauzo mengi kinachoangazia ukweli wa kushangaza na mafanikio yasiolingana

10. Gary, John. “Ten Global Trends in Religion.” [wnrf.org <http://www.wnrf.org/cms/tentrends.shtml>](http://www.wnrf.org/cms/tentrends.shtml) 17 July 1997.

11. Huntington, Samuel P. *The Clash of Civilizations and the Remaking of World Order*. New York: Simon & Schuster, 1996. pp. 65-66.

12. *Guinness Book of Knowledge*. p.195. [Kwa ushahidi zaidi kuonesha Uislamu ni dini inayokua kwa kasi soma: Baum, Geraldine. “For Love of Allah.” *Newsday* Nassau and Suffolk Edition, Part II, 7 March 1989: p.4 ; Goldman, Ari L. “Mainstream Islam Rapidly Embraced by Black Americans.” *New York Times* Late City Final Edition, 21 Feb. 1989: p.1; Kopel, Ted. *Nightline* ABC. April. 1998; Young, Gayle. “Fast-growing Islam winning converts in Western world.” [cnn.com](http://edition.cnn.com/WORLD/9704/14/egypt.islam/) 14 April 1997 <<http://edition.cnn.com/WORLD/9704/14/egypt.islam/>>; Blank, Jonah. “Islam is growing fast in America, and its members defy stereotypes.” *US News* 12 July 1998. <http://www.usnews.com/usnews/news/articles/980720/archive_004363.htm>; Seitz, Barr. “Fastest-Growing Religion Often Misunderstood.” *BICNews*. ABC. 13 Dec. 1997; Robinson, B.A. “University Dispute re: Islamic Book.” [religioustolerance.org](http://www.religioustolerance.org/isl_unc.htm) <http://www.religioustolerance.org/isl_unc.htm> 17 Aug. 2002 ; Ali, M.M. “Muslims in America: The Nation’s Fastest Growing Religion.” *Washington Report on Middle East Affairs* May/June 1996. pp. 13, 107.]

ya kibinaadam, kinasema, “Katika kipindi cha 1990 mpaka 2000, takriban watu wapatao milioni 12 na unusu walibadili dini kuuelekea Uislam kuliko Ukristo”, kwa akili yenye udadisi mkubwa itahitaji maelezo na kutokana na hilo hii ni ambalo *Guinness World Records 2003* ilirikodi:

Uislam ndio dini ieneayo kwa kasi zaidi, Mnamo mwaka 1990, watu milioni 935 walikuwa Waislam na idadi hii ikaongezeka hadi kufikia bilioni moja na laki mbili mwaka 2000, ikimaanisha mmoja kati ya watano duniani tayari ni Waislam. Ingawa dini hii ilianza(tukiongelea kipindi cha Muhammad) Uarabuni, mpaka mwaka 2002, asilimia 80 ya waumini wake wako nje ya uarabuni. Katika kipindi cha 1990-2000, takriban watu milioni 12 na nusu wameingia katika Uislam zaidi kuliko wale walioingia katika Ukristo.”¹³

Hermann Eilts (aliyezaliwa mwaka 1922) aliyekuwa balozi wa Marekani Saudia Arabia na Misri ambaye baadae akajiunga na Chuo Kikuu cha Boston kama Profesa wa Masuala ya Kimataifa (International Relations), na hapo kuwa mkuu wa kitengo cha Sayansi ya Siasa (Political Science) na baadae kuwa mkuu wa kitengo cha Masuala ya Kimataifa alikuwa na haya ya kusema:

13. *Guinness World Records 2003*. p. 102. Pia katika *Guinness World Records 2004* p.90. Katika ukurasa wake kuelezea haki za kunakili, kuna onyo madhubuti lililosema: “Kujaribu kuvunja rikodi au kuweka rikodi katika jambo Fulani ni hatari sana. Umakini na uangalifu wa hali ya juu unahitajika katika kuliendea hilo na kama lolote likikutokea basi dhima itakuwa ni yako mwenyewe. Kwa njia yeyote ile, kampuni ya Guinness World Records haitahusika na kifo au madhara yoyote yatakayojitokeza kutokana na kujaribu kuweka rikodi duniani.” Hapo ndipo mtu atapopigwa na butwaa na kujiuliza hivi hizi dini nyengine zinajua yatakayo yakuta kwa kujaribu kuipiku rikodi ya Uislamu ya kuwa dini inayokuwa kwa kasi zaidi duniani.

“Waislam duniani sasa wamekaribia billion moja*,hiyo ni takwimu ya kuvutia. Lakini kwangu mie linalovutia na kushangaza zaidi ni Uislam kuwa dini ikuayo kwa kasi zaidi katika dini zinazoabudu Mungu mmoja. Hili ni jambo lazima tulitilie mkazo. Kutakuwa na jambo la kweli kuhusu Uislam kwani watu wengi wamekuwa wakivutika.”¹⁴

Hawa Ima ni Waerevu au Wajinga

Sasa na tuangalie kwanini hawa watu wengi kama tutavyowaona wanakana imani zao na kuamua kuupokea Uislam, japokuwa wanakutana na vita ya kuzingatia dini hii kali na matokeo magumu kwao. Je! Hawa waliosilimu hawakuona kama sheria za Kiislam zinazotakiwa kuja kutawala dunia kuwa ni za kibaguzi, za kinyama, na za kikatili?! Hawaoni kama ni dini ngumu na kali sana isiyoendana na dunia ya sasa?! Mtu yampasa aamke kabla ya alfajiri kuswali moja ya swala tano za kila siku. Kufunga mwezi mzima kila mwaka! Kusafiri kwenda Saudi Arabia kwa ajili ya Hijja japo mara moja katika maisha yako. Kinachoonekana kushangaza ni kuwa mtu anahiji yampasa amrushie mawe shetani! Mwanamke anatakiwa kujifunika kuanzia kichwani mpaka kwenye vidole vya miguu, bila kuzingatia miguu yake mizuri na hali ya hewa ya joto. Na wewe kama ni mwanamke wa Kiislam, inakuwaje mmeo anao uwezo wa kukuletea mke mwengine. Uislam unampa haki isiy

* Hiyo ilikuwa Juni 24, 1985, kwa sasa Waislamu wanafikia bilioni moja na nusu, angalia, “The Bible v the Koran, the battle of books.” *The Economist* 22 Dec. 2007.p.62. Pia tazama katika, “Major Religions of the World Ranked by Number of Adherents.” [adherents.com](http://www.adherents.com/Religions_By_Adherents.html) <http://www.adherents.com/Religions_By_Adherents.html> last retrieved 2 June 2009. ; na kutokana na jarida la *Time*, “Moja ya sababu ya kukua kwa uchumi halal ni hii idadi ya vijana bilioni 1.6 ambao sehemu zengine ni matajiri kuliko.” Tazama Power, Carla. “Halal: Buying Muslim.” *Time* 25 May 2009. p.38. Sanjari na hilo, Taasisi ya *Pew Forum on Religion & Public Life* ilifanya utafiti mkubwa mwaka 2009 na kukuta Waislamu duniani wakifikia bilioni 1.57. Tazama, *Pew Forum on Religion & Public Life*. “Mapping the Global Muslim Population: A Report on the Size and Distribution of the World’s Muslim Population.” 8 Oct. 2009; Beaumont, Peter. “One in four people is Muslim, says study.” *Guardian* 8 Oct. 2009.

14. Katika hotuba kwa kamati ya mambo ya nje katika bunge la Marekani Juni 24, 1985

ya kawaida ya kuoa mpaka wake wanne. Utahofishwa zaidi pale utapogundua Uislam umempa haki mme kumwadhibu mkewe kwa viboko kama akiwa hatii [Q 4:34]. Mtu atauliza, “Hivi hawa wanawake wanaoingia katika Uislam hawahofii kufanywa kama wafu kwa kuvalishwa maguo kutoka juu mpaka chini na bado huyu mwanamke hahofii pale mme wake mwenye wake wengi anapompa ujauzito wa watoto sita kwa wakati mmoja (sextuplets)?!

Kuwa Muislam yapasa utoe zakaat kutoka katika kiasi chako cha fedha ulichokipata kwa tabu na mashaka. Yaani asilimia mbili na nusu (2.5%) ya mahifadhi yako ya mwaka yanaenda kwa maskini! Halafu usijaribu kuiba; mkono wako wataukata [Q 5:38]. Tumeshambuliwa na matangazo ya pombe halafu Qur'an inatuambia kuwa pombe ni kazi ya shetani [Q 5:90], na hivyo yapasa kujiepusha nayo, kwa yote haya ataishi vipi huyu?! Na kabla ya moyo kutulia kutokana na mshtuko ulioupata, bado unaambiwa sandwich (hambaga) uipendayo zaidi yenye nyama ya nguruwe katikati ni haramu katika Uislam! Na isitoshe, hairuhusiwi kusilikiza miziki au kutazama MTV! Linachosha zaidi basi dini yenyewe imeongozwa na Muhammad “...Mtume, Nabii *Ummu* (asiyejua kusoma wala kuandika...)” [Q 7:157] Hivi wataweza kumuiga Muhammad, mfano wao wa kuigwa kwa kusugua meno yao kwa kutumia mti (miswak)! Vipi basi hawa wastaarabu, wavumilivu na wapenda amani wamfate Mtume huyu ambaye alisema “... Nimefanywa mshindi kwa (maadui zangu kupewa) uwoga [yaani Mwenyezi Mungu amefanya maadui wa Uislamu wamuogope Mtume hata kabla ya mapambano]....”¹⁵ mtu huyo huyo aliyeshinda anawajaza roho ya Jihad wafuasi wake wakikumbana na maadui wa Uislam tangia Allah alivyomuamrisha “Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu)! Wahimiza walioamini (Waislamu) wende vitani.” [Q 8:65]. Hivi hawaoni kuwa Muhammad kaamsha hofu zaidi, chuki na dharau kubwa kwa Wakristo ulimwenguni kuliko mtu yeyote aliyewahi kutokea?”¹⁶

15. Bukhari Vol. 4, Bk. 52, No. 220.

16. Hofmann, Murad Wilfried. *Religion on The Rise: Islam in the Third Millennium*. Maryland: Amana Publications, 2001.p. 54

Inakuwaje hawa wanaosilimu wanakubali kumuabudu Mungu wa Waislam aliyesema, “...Nitatia woga katika nyoyo za makafiri...”[Q 8:12] Na kama hiyo haitishi angalia Mungu huyo huyo anawaamrisha Waislam katika mapambano “...Basi wapigieni (kwa panga) juu ya shingo (zao) na kateni kila ncha za vidole vyao.”[Q 8:12] Inakuwaje uonevu wote huo? “Hayo ni kwa sababu wamemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake.”[Q 8:13] asema Mungu wa Waislamu. Na isisahaulike kuwa dunia kiUislam imegawanyika katika “nyumba ya Uislam (Dar al-islam)” na “nyumba ya vita(Dar al-harb)”. Mgawanyo huo utamstajabisha mtu: Kwani Uislam ni dini ya uvamizi na kukamata nchi nyengine kwa nguvu? Kufanya vitu viwe vibaya zaidi, wale wote waliosilimu wanatakiwa waelewe kuwa wale ndugu, jamaa na marafiki waliowaacha walipotoka wao sio zaidi ya kuwa ni makafiri tu.*

* Kafir inamaana ya yule anayepinga. Kwa maana ya Kiislamu, Kafir ni mtu anayepinga ukweli wa Uislamu (kwa kizungu Non-muslim). Kiufupi, Kafir ni mpingaji. Hujawahi kupinga kuisoma Qur'an, kusoma vitabu vya Kiislamu au kusikiliza mafundisho ya Uislamu. Je huo sio upingaji? Na kama umepinga kuisoma qur'an kwanini ulalamike endapo Muislamu akikuwa ni Kafir? Baada ya kuisoma hiyo Qur'an kuna mambo unaweza kuyapinga, je huo sio upingaji tena? Ni jambo sahihi kabisa kumuita Muislamu hivyo hivyo iwapo atayepinga Yesu Kristo ambaye katajwa katika vitabu vya Mungu kama Qur'an na Injili. Kwanini imani zengine zinahisi kukashifiwa kama wakiitwa makafiri na Waislamu kwa kupinga kumkubali Muhammad! Je ikatokea wasio Wakristo wakaikwa makafiri na mungu wa Biblia, je Wakristo watamuhoji mungu wao kwa hilo? Mungu ndio kashawaita wasio Waislamu kuwa ni makafiri na jambo la msingi hapa ni kujiuliza kama kweli hii Qur'an ni neno la Mungu! Kama ni neno la Mungu basi, “Ole wake ashindanaye na Muumba wake! Kigae kimoja katika vigae vya dunia! Je! Udongo umwambie yeye au finyangaye; Unafanya nini? Au kazi yako, Hana mikono?” [Isaya 45:9]. Cha kushangaza Qur'an inakazia mkazo kauli hiyo kuwa siku ya kiyama, na wasio Waislamu watakubali na kujiita wenyewe ni makafiri. Aya inasema: “Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakukujieni Mitume kutokana na nyinyi wenyewe wakikubainishieni Aya zangu, na wakikuonyeni mkutano wa Siku yenu hii. Nao watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Nao watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri.” [Q 06:130; pia tazama Q 7:37] Mtume wa karne ya nane; Amosi anawaita wale wanaokataa sheria za Mungu kuwa ni ‘ngo'mbe’ [Amosi 4:1] na Mtume Yeriahi anawaita watu hao ‘waovu’ (scoundrels) [Yeriahi 5:26], Yesu anawaita waovu hao kuwa ni ‘wazao wa nyoka’ [Mathayo 12:34] na katika mahala kwengine aliwaita ‘kizazi kibaya na cha zinaa’ [Mathayo 16:4] Waislamu wa sasa kwa huruma zao kwa hawa waovu wanaokataa sheria za Mungu, hawawaiti ‘ngo'mbe’, ‘wazao wa nyoka’, wala ‘kizazi kibaya na cha zinaa’ bali wamebaki kuwaita makafiri tu yaani wapingaji.

Ukiwa Muislam unapewa jina jipya: Gaidi! Kubadilika kuwa Muislam kunamaanisha kutia hasira na kuondoa utulivu kwa familia, marafiki, jamii, serikali na hata mashirika ya kimataifa! Wakati mwingine, kuacha sifa na heshima yako, na hata uwezekano wa kuachishwa kazi yako pia! Kwanini waume kwa wanawake hawa waendeleo kuikumbatia dini ambayo inaambatanishwa na serikali za kidekteta, ugaidi, unyanyasaji wa kijinsia, video za kukata watu vichwa, na imani yao ya kusambaza dini kwa upanga?! Na cha kushangaza zaidi, sheria yao imetoa kibali cha kuuliwa kwa yeyote aliyeasi (aliyeritadi) kisa tu Muhammad kasema: “**Kama Muislam ataiacha dini yake, muueni.**”¹⁷ Lakini bado waume kwa wake wamekuwa wakiipokea dini hii. Wale tu waliozidi ujinga au waliozidi uwerevu ndio wangechukua uamuzi huo.* Lakini nani afahamuye, yawezekana uamuzi wao umekuwa rahisi sasa kwa kuwa utashi wao wa kumridhisha Mungu umezidi ule wa kuiridhisha dunia.

17. Bukhari, Vol. 4, Bk. 52, No. 260. Pia angalia, Bukhari Vol. 9, Bk. 83, No. 17. Na pia kutokana na hiyo hiyo Bukhari Vol. 9, Bk. 89, No. 271, kulikuwa na mtu ambaye alisilimu na baadae kurudi katika Uyahudi. Mu’adh bin Jabal, swahaba wa Mtume ambaye alipata kumuona mtu huyo na Abu Musa, swahaba mwingine wa Mtume. Mu’adh akauliza ana nini huyu mtu? Abu Musa akamjibu, “Alisilimu kasha akarejea katika uyahudi.” Mu’adh akasema, “Sitakaa chini mpaka uwe ushamuu huyu mtu kama alivyosema Allah na mjumbe wake”.

* Kuna kueleweka ndivyo siyo kwingi dhidi Uislamu. Hata hivyo kwa wale wanaonesha dira ya kutaka kuujua ukweli basi wanashauriwa walau wakisome kitabu cha Dkt. Zakir Naik, *Answers to Non-Muslim common Questions About Islam (Majibu kwa Maswali Yaliyozeleka kwa Wasio Waislamu Kuubusu Uislamu)*. Dkt. Zakir Naik ni mhubiri fasaha wa kimataifa wa Kiislamu. Ni mwanzilishi na rais wa Islamic Research Foundation (IRF). Kwa egemeo la maandiko (Qur’an, Biblia n.k) na utumizi wa akili ya kawaida, mantiki na sababu za kisayansi, Dkt. Zakir amefanikiwa kufuta uelewa huo mbovu wa Uislamu. Katika kitabu hicho, utaona majibu yanayoridhisha katika maswali kama kwanini Waislamu wana mume wanaruhusa ya kuoa zaidi ya mke mmoja? Kwanini Uislamu unawashusha thamani wanawake kwa kuwavalisha hijab? Kwanini Waislamu wengi ni magaidi? Kwanini pombe ikatazwe katika Uislamu? Na kwanini Waislamu wawakashifu wasio Waislamu kwa kuwaita makafiri? N.k unaweza kupata kitabu hiko bure kutoka mtandaoni : <<http://www.islambasics.com/view.php?authID=154>>; Also see <<http://www.ilovezakirnaik.com/misconceptions/index.htm>>

Kuyakataa Mabaya na Kuyachagua Mema

Wengi ya hawa waliorudi* katika Uislamu wanayo taarifu katika Biblia yao isemayo “...kuyakataa mabaya na kuyachagua mema”. [Isaya 7:15], lakini bado wameuchagua Uislam. Kitakachojalisha kama chaguo lao ndio bora na jema ni kina cha utafiti walichochimba na mashiko waliyoyashika ambayo kwa kebehi kubwa yanadharaulika na wengine. Ukifikiria kama walitumia sababu, dalili na uwazi wa akili katika tafiti zao basi bila shaka watakuwa wamechagua chaguo zuri kama alivyosema Thomas Jefferson “Sababu na uchunguzi wa wazi ndio njia pekee za kushinda makosa”. Waliupata ukweli kwa kufatilia na kuudadisi au waliamua kukubali (shingo upande) kurithishwa dini na wazazi kama tu vile alivyokuwa mtoto akifyonza maziwa ya mzazi (mama) basi naye akafyonza kila kitu mpaka dini ya mzazi (mama) pia!!? Ni kweli usiopingika kuwa, ukweli siku zote ndio utakaokuweka huru lakini ukweli huo lazima uwe unaokubalika na wengi, hata kama kwa wakati mwingine uko nje ya mipaka ya dini au jamii. Hi ndio sehemu ngumu zaidi kama asemavyo Galileo, “Ukweli wote huwa ni rahisi kuuelewa pale utapogundulika, tatizo ni hapo katika kuugundua”. Inawezekana hawa waliosilimu waliweza kumpata Mungu baada ya kuufata ushauri wa Biblia, “Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.” [Yeremia 29:13], katika hii sehemu ya mwisho ya mstari yaani “mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote”, ni kumaanisha kutafuta dini ya kweli kwa

* Ingekuwa haturithi dini kutoka kwa wazazi wetu, ipi unafikiri ingekuwa dini yetu ya kufata? Bila shaka tungeifata ile dini inayokubaliana na sheria za kuzaliwa za Mungu kwa binadamu. Sasa kama umerithi kutoka kwa wazazi ubudha na ukaamua kuingia katika Uislamu basi utakuwa umerudi katika dini yako ya asili. Kutoka katika vyanzo vya Kiislamu, kila binaadamu huwa anazaliwa Muislam, na ndio maana tumetumia neno kurudi katika Uislamu. Mtume alisema, “Hakuna mtoto aliyezaliwa ila alikuwa Muislamu kisha ni wazazi wake ndio wanaomfanya awe myahudi, mnaswara au mshirikina.” [Muslim, Bk. 33, No. 6426]. Ali Mazrui, mwanasayansi mashuhuri wa siasa anaandika, “...Marekani kwa mara ya kwanza wamechagua mtoto wa Muislamu kuwa Rais. Hivyo ndivyo alivyokuwa baba yake japokuwa alikuwa mlevi. Hii inamaanisha Obama alizaliwa kama Muislamu japo baadae akalelewa Kikristo...” Tazama Mazrui, Ali. “Obama has chance to mend US-Muslim relations.” City Press 13 Dec. 2008.

utulivu, umakini, juhudi na ari ukiondoa upendeleo . . . kama vile kusoma Qur'an aya baada ya aya, na kusoma vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni waheshimiwa Wakiislam....Lakini kwa bahati mbaya hitajio la ukweli ni dogo kuliko usambazaji wake.Lazima utashangaa, sasa vipi mtu anaweza kuwa huru katika kuujua na kuufata ukweli? Wale ambao wanaamua kwa furaha na majigambo kukana kufanya uchunguzi wa ukweli wa Uislam, inabidi angalau wayafikirie maneno ya Joanne Kathleen Rowling, mwandishi wa Kiingereza na mtunzi wa Harry Potter, “Kutofautiana na kutelekezwa kwa dharaui huwa inaleta madhara makubwa kuliko hata kutopenda (chuki) kabisa”. Labda hawa waliosilimu walikuwa na aina ya uhuru iliyozungumziwa na C. Wright Mills wakati aliposema, “Uhuru sio kabisa ile nafasi ya kuchagua kile utakacho, wala pia sio ile nafasi ya kuchagua baina ya pande mbili bali uhuru ni kwanza kabisa ni ile nafasi ya kujitengenezea machaguo, kuyajadili na halafu ndio uchague.”

Wakati tukisema watu wanazidi kuupokea Uislam siku hadi siku huwa tunamaanisha na kuongelea wasomi wa Ukristo, matajiri, watu maarufu, watu wenye nguvu, wasomi wakubwa, masista wa kanisani, wachungaji, wenye kushawishi watu kuingia Ukristo (evangelicals), marabi, na wale wachaji Mungu katika dini tofauti tofauti bila kuwasahau wale wasio na uwezo katika jamii.* Kuongezea nguvu yaliyosemwa hapo juu, tafti Fulani ya waliobadili dini kuingia katika Uislam kama ilivyoripotiwa na gazeti la *The Sunday Times* la 22 Februari 2004 inaonesha wamiliki ardhi wakubwa wa uingereza, watu mashuhuri na watoto wa wakubwa wameupokea Uislam baada ya kuvunjwa

* Ikumbukwe kuwa wengi kati ya wafuasi Muhammad walikuwa ni wale watu wa chini katika jamii mathalan watumwa, mafukara, wanaokanyagwa na wengineo. Na mfano huu umezungumziwa na Heraclius katika kuujua ukweli wa dini. Hivi ndivyo Heraclius alivyodadisi: “Nilipokuuliza ‘Je wengi wanaomfuata huyo Mtume Muhammad ni maskini au matajiri?’ Ukajibu kuwa ni maskini ndio wanaomfuata. Ama kweli, wafuasi wa Mitume wa kweli walikuwa ni maskini.” [Angalia, Bukhari Vol.4, Book 52, Hadith Number 191.]

moyo na maadili ya kimagharibi.¹⁸ Kiufupi, watu kutoka nyanja zote za maisha, huwa wanaamua kuukubali Uislam bila jitihada kubwa wala shughuli kubwa za kimishenari.

Kiuhalisia, ni Waislam wachache mno wanaoweza kuuacha Uislam kwa ajili ya Ukristo au dini nyengine. Wengi wa hawa waasi wa Uislam, huwa ni ama wazaliwa katika Uislamu lakini wasioijua dini ya Kiislam (wajinga) na hawajajifunza; wafuasi wa madhehebu potofu ya Kiislam; waliotawaliwa na kushawishika na vitu vya kidunia; wasio na mazingira ya kuusoma Uislam; masikini ambao hawana jinsi ila kuvutika kupitia msaada wa msamaria wa Kikristo; wale ambao “...Mwenyezi Mungu ameziziba nyoyo zao na masikio yao na macho yao. Na hao ndio walio ghaflika.” [Q 16:108] na wale wanarubuniwa kiakili. Kwa kulinganisha, wasio Waislam ndio wengi wanaoingia katika Uislam kuliko hao Waislam ambao ni nadra kuwaona wakiaacha dini yao na kuingia nyengine. Cha kushangaza sasa, huwezi kusikia mcha Mungu, mfuasi, sunni wa Kiislam aliyeshiba maarifa ya Uislam akiiacha dini yake eti kwa ajili ya dini nyengine. Ukijumuisha fedha zote walizo nazo, njia na uwezo wa kisasa, na zenye mipangilio mizuri watumiazo katika shughuli na jitihada zao za kimishenari, bado Ukristo hauwezi kuwaopoa Waislam katika dini yao kama vile Waislam wanavyowakomba Wakristo. Sanjari na hilo Peter Kreeft, mtetezi wa Kikatoliki, profesa wa falsafa katika chuo cha Boston na The King's College, mtunzi wa vitabu zaidi ya 45, msomi na mzungumzaji anayehitajika katika makongamano mbalimbali, na pia ni mjumbe wa bodi ya ushauri wa Kituo cha Watoa Elimu cha Kikatoliki (Catholic Educator's Resource Center) anasema: “Uislam una kiwango kidogo cha kupoteza waumini wake na kiwango kikubwa sana cha kuingiza waumini”.¹⁹ Hilaire Belloc (1870-1953) ni Mkatoliki, mwanahistoria mzawa wa Ufaransa, na mmoja kati waandishi wenye vitabu vingi Uingereza alikumbana

18. Hellen, Nicholas and Christopher Morgan. “Islamic Britain lures top people.” *The Sunday Times* 22 Feb. 2004. Also see: Whittell, Giles. “Allah Came Knocking At My Heart.” *The Times* 7 Jan. 2002.

19. Kreeft, Peter. “Comparing Christianity & Islam.” *National Catholic Register* May 1987.

na kimbembe cha ugumu wa kuwatoa Waislam kutoka katika dini yao, hiyo ikiwa ni mnamo mwaka 1938:

“Uislam ni dhahiri haubadilikiki. Jitihada za kimeshenari zilizofanywa na Wakatoliki ambazo zimekuwa na dhima ya kuwahamisha wafuasi wa Muhammad kwenda katika Ukristo kwa miaka takriban 400 kwa hakika zimefeli. Tumeweza kumuondoa kiongozi wa Kiislam baadhi ya sehemu na hivyo kuwarudisha watu wetu waliokuwa wametawaliwa na viongozi kama hao wa Kiislam, lakini tumeshindwa kuwavuta wale Waislam* wenyewe mmoja baada ya mwengine....”²⁰

Takwimu Zitaongea kwa Sauti Zaidi

Tunaamini takwimu nyingi zitaongea kwa sauti yenye kusikika zaidi kuliko maneno tu ambayo tuliyokuwa tunayatumia. Kama ilivyonukuliwa kutoka katika Kamusi-elezo ya Kikristo ya Dunia (*World Christian Encyclopedia: A Comparative Study of Churches and Religions in the Modern World*) ikielezea tafiti ya makanisa na dini katika dunia hii ya sasa inasema:

“...Ukristo umepata upungufu mkubwa wa wafuasi katika pande la magharibi mwa dunia na katika nchi za kikomonisti kwa miaka 60 iliyopita. Katika Muungano wa Kisovieti (sasa Urusi), Wakristo wamepungua kutoka asilimia 83.6 mwaka 1900 mpaka kufikia asilimia 36.1 leo hii. Ulaya na Marekani ya Kaskazini, usaliti kutoka Ukristo kuingia katika dini nyengine

* Uislam ndio dini pekee yenye lisilotokana na mtu au kabila. Uislam una maana ya kunyenyekea kwa Allah tofauti na ukristo ulioitwa baada ya Yesu kristo, Budha baada ya Gotama Buddha, Ukonfyushasi baada ya kumfata mwanafalsafa wa kichina Confucius, Umaksi baada ya kuwa wafuasi wa Karl Marx. Na hata dini kama Uyahudi na hindu ni baada ya ya makabila ya yahudi na uhindi.

20. Belloc, Hilaire. *The Great Heresies*. New York: Sheed & Ward, 1938. p. 98.

au kutokuwa na dini kabisa zimefikia 1,820,500 kwa mwaka. Hii ni hasara na upotezaji mkubwa....”²¹

Kulingana na jarida la Kikristo, *The Plain Truth*,²² ambalo vyanzo vyake ni *World almanac* na *Book of Facts* 1935, *Reader's Digest Almanac* na *Yearbook* 1983, linatutanabaisha kuwa katika kipindi cha miaka hamsini (1934-1984):

Ukristo umeongezeka kwa asilimia 47%

Idadi ya watu duniani imeongezeka kwa asilimia 136%

Na Uislam umeongezeka kwa asilimia 235%

Kutokana na takwimu tulizozipata katika jarida hilo, kama tukachukua dini tatu tu jedwali litakuwa kama ifuatavyo:

	Idadi ya wafuasi mwaka 1934	Idadi ya wafuasi mwaka 1984	Ongezeko la asilimia
Uislam	209 020 000	700 000 000	235% Ongezeko
Ukristo	682 400 000	1 000 000 000	47% Ongezeko
Uyahudi	15 630 000	15 000 000	4% Punguzo

Makala iliyokuwa katika jarida la *The Plane Truth* la mwaka 1984 ilisema, “Kinyume na kupungua kwa waumini makanisani huku Magharibi, habari zinaripti mwenendo na maendeleo ya Waislam yaliyo kinyume kabisa na sisi. Uislam unaweza kuwa ndio dini itakayokuwa na kuenea zaidi duniani....”²³ Na ni kweli kama ilivyotabiriwa, Uislam sasa ndio dini yenye kukua kwa kasi zaidi duniani. Hata Vatikani wanaukubali ukweli huo kuwa

21. Barrett, David B. World Christian Encyclopedia: A comparative study of churches and religions in the modern world, AD 1900-2000. New York: Oxford University Press, 1982.p. 7.

22. Stump, Keith. W. “A Crucial Half Century of Religion.” The Plain Truth Feb. 1984 p.11.

23. Stump, Keith. W. “A Crucial Half Century of Religion.” The Plain Truth Feb. 1984 p.20.

sasa Uislam umeupiku Ukatoliki, “Kwa mara ya kwanza katika historia, hatupo tena juu; Waislam washatupiku,” haya yalisemwa na Monsignor Vittorio Formenti katika mahojiano yake na gazeti la vatikani *L'Osservatore Romano*. Formenti ambaye ndiye mkusanyaji na mpangaji makala katika kitabu cha Vatikani cha kila mwaka alisema Wakatoliki wamefikia asilimia 17.4 ya watu wote duniani- asilimia isiyooongezeka- wakati Waislam washafika asilimia 19.2 sasa.²⁴

Sanjari na hilo, *The World Christian Database* (WCD) na wale watangulizi wao *World Christian Encyclopedia* (WCE - *Kamusi Elezo ya Kikristo Duniani*) walifanyia utafiti wa idadi ya watu katika masuala ya kidini na kuachia matokeo ya chunguzi zao kwa mara kadhaa. Kutoka katika majedwali ya matokeo yao, malingano ya Ukristo na Uislam katika ukuaji yalikuwa kama ifuatavyo:

Asilimia ya Ukuaji kwa Mwaka			
	{1970-1985}	{1990-2000}	{2000-2005}
Uislam	2.74%	2.13%	1.84%
Ukristo	1.64%	1.36%	1.38%

[Rejea za takwimu zilizotolewa fatilia katika: Barrett, David B., George Thomas Kurian, and Todd M. Johnson. 2001. World Christian Encyclopedia: A comparative survey of churches and religions in the modern world. New York: Oxford University Press. p 4. Pia pitia, “The List: The World’s Fastest-Growing Religions.” Foreign Policy 14 May 2007.]

24. Richard Owen. “Islam overtakes Catholicism as world’s largest religion.” Times 31 March 2008; also see Kington, Tom. “Number of Muslims ahead of Catholics, says Vatican.” The Guardian 31 March 2008; “Muslims outnumber Catholics.” PRESS TV. 30 Mar 2008 < <http://www.presstv.ir/detail.aspx?id=49503§i onid=3510212>> ; Rizzo, Alessandra (Associated Press Writer). “Muslims More Numerous Than Catholics.” ABC News 30 March 2008; CBS News 30 March 2008.

Akielezea dini zisizikuwa za Kikristo, msimamo wa mtunzi wa WCE ni: "...tunaweza amini kuwa dini hizo ni za uongo na hazifai na tukajaribu kuzivuta katika imani ya Yesu Kristo..."²⁵ tukiamini kuwa takwimu hizi za 'dini pingaji' hazina upendeleo na haziko kwa ajili ya kuwashinda kuwavuta kuingia katika imani ya Yesu Kristo, wacha sisi tuzitumie katika uchambuzi wetu. The *World Christian Encyclopedia* inatupa idadi ya wote Waislam kwa Wakristo ya mwaka 1900 na ya mwaka 2000. Idadi ya Wakristo mwaka 1900 ilikuwa na 558 056 332 na mwaka 2000 ikawa 2 019 921 366 na idadi ya Waislam katika miaka hiyo hiyo ilikuwa 200 102 284 na 1 200 653 040.²⁶

Kanuni rahisi ya kukokotoa asilimia ya ongezeko katika vipindi hivi ni hii ifuatayo:

$$\text{Ongezeko la Asilimia} = \frac{\text{Idadi ya Sasa} - \text{Idadi ya Mwanzo}}{\text{Idadi ya Mwanzo}} \times 100$$

Sasa, tukitumia takwimu tulizopewa kutoka WCE, tutapata ongezeko la Wakristo kiasilimia litakuwa:

$$\text{Ongezeko la Asilimia} = \frac{2\,019\,921\,366 - 558\,056\,332}{558\,056\,332} \times 100$$

Na baada ya kukokotoa, ongezeko la Wakristo litakuwa **262%**

25. Barrett, David B. Preface. *World Christian Encyclopedia: A comparative study of churches and religions in the modern world, AD 1900-2000*. By Barrett. New York: Oxford University Press, 1982.

26. Barrett, David B. *World Christian Encyclopedia: A comparative study of churches and religions in the modern world, AD 1900-2000*. New York: Oxford University Press, 1982.p. 6.

Tukifanya mahesabu hayo hayo kutumia idadi ya Waislam katika vipindi hivyo.

$$\text{Ongezeko la Asilimia} = \frac{1\,200\,653\,040 - 200\,102\,284}{200\,102\,284} \times 100$$

Tutapata ongezeko la Waislam kuwa ni **500%**

Bado, Uislam unaongoza kwa kuwa na asilimia 500% na Ukristo kuwa na 262%. Mwaka 1997, mwanatakwimu kutoka *US Center for World Mission* alisema kuwa kiujumla idadi ya wafuasi wa Kikristo inaongezeka kwa asilimia 2.3 kila mwaka.²⁷ Kutokana na *Ontario Consultants on Religious Tolerance* Uislam unakuwa kwa asilimia 2.9 kila mwaka ambaye ni kasi kubwa kuizidi kasi ya ongezeko la idadi ya watu duniani ambayo ni asilimia 2.3 tu kwa mwaka.²⁸ Tukichunguza na kufikiri kwa makini, hakuna ugumu utakaibukia katika kukubaliana kuwa kwa mwenendo huu wa Uislam, karibuni kitafika kipindi ambacho Uislam utakuwa ushazivuka dini zote ulimwenguni. Mnamo mwezi Oktoba 2009, gazeti la Kenya *The Standard* liliibuka na makala ilobeba ujumbe: “Mmoja katika kila wanne ni Muislam katika kipindi hiki ambapo wafuasi washafikia bilioni 1.57 duniani.”²⁹ Takwimu hizi ziliwekwa hadharani na Pew Forum on Religion & Public Life katika ripoti yao ambayo inaheshimika kwa machangunuo ya kinagaubaga kuliko zote inazofanana nazo. Kama mwaka 2000,

27. Greg H. Parsons, Executive Director, U.S. Center for World Mission, Pasadena, CA; quoted in Zondervan News Service, 21 Feb. 1997.

28. Robinson, B.A. “Growth Rate of Christianity & Islam.” [religioustolerance.org](http://www.religioustolerance.org/growth_isl_chr.htm) 6 Nov. 2001. <http://www.religioustolerance.org/growth_isl_chr.htm>; Pia tazama, Khan, Arshad. *Islam, Muslims and America: Understanding the Basis of Their Conflict*. Algora Publishing, 2003.p.29.

29. Gorski, Eric (AP Religion Writer). “One in every four is a Muslim as followers hits 1.57 billion worldwide.” *The Standard* 9 Oct. 2009. Pia tazama, Greene, Richard Allen. “Nearly 1 in 4 people worldwide is Muslim, report says.” *CNN* 8 Oct. 2009; <<http://edition.cnn.com/2009/WORLD/asiapcf/10/07/muslim.world.population/index.html>>; Beaumont, Peter. “One in four people is Muslim, says study.” *Guardian* 8 Oct. 2009; *Pew Forum on Religion & Public Life*. “Mapping the Global Muslim Population: A Report on the Size and Distribution of the World’s Muslim Population.” 8 Oct. 2009.

WCE walisema Waislam walikuwa bilioni 1.2 na baada ya miaka tisa tu Pew Forum waseme Waislam washafika bilioni 1.57. vipi idadi ya Waislam itakuwa baada ya miaka hamsini?! Na tushubiri tuone.

Uislam Unakuwa kwa Watu Kusilimu

Ni muhimu kuelewa kuwa Uislam haukui kwa kiasi cha kuzaliana sana Waislam tu bali vile vile kwa watu kuupokea na wakaukubali. Marekani pekee, kutokana na gazeti la *St. Petersburg Times*, “Kila mwaka Marekani, takriban watu 20, 000 wanaingia katika Uislam, ukiachia wale wanaosilimia katika gereza..., halafu hawa wanaosilimu, wengi wao ni wanawake, na tena wengi katika hao ni vijana ambao bado hawapo katika ndoa...”³⁰ Shirika la habari la *NBC* liliripoti idadi hiyo hiyo ya wafuasi wa dini zengine wanaoingia katika Uislam mwaka hadi mwaka. Na kutokana na gazeti la *New York Times*, “Karibia asilimia 25 ya Waislam Wamarekani ni waliosilimu.”³¹ Uingereza, gazeti la *The Times* liliripoti, “. . . katika idadi isiyo na kifani ya Waingereza, wengi wao wakiwa wanawake, wanaingia katika Uislam . . .”³² Na mwaka 2004, *The Sunday Times* lilisema, “. . . zaidi ya wazungu (waingereza) 14,000 washaingia katika Uislamu. . .”³³ japokuwa, kutokana na utafiti wa kina uliofanywa na Kevin Brice wa Chuo Kikuu cha Swansea, inakadiriwa kuwa mwaka 2010, kulikuwa na Waingereza (wazungu) 100,000 waliosilimu Uingereza “. . . kukiwa na zaidi ya

30. Wiener, Jocelyn (Times Staff Writer). “Young, Female and Muslim.” *St. Petersburg Times* 7 Oct. 2002.

31. Elliott, Andrea. “Muslim Converts Face Discrimination.” *New York Times* 30 April 2005.

32. Berrington, Lucy. “Why Are British Women Turning to Islam?” *The Times* 9 Nov. 1993.

33. Hellen, Nicholas and Christopher Morgan. “Islamic Britain lures top people.” *The Sunday Times* 22 Feb. 2004.

watu 5,000 wabadilikao, kila mwaka kitaifa.”³⁴ Utafiti huo ulifanywa na the inter-faith think-tank, iitwalo Faith Matters. Kusema kweli takwimu hizi zinatuhabarisha jambo fulani kuhusu muelekeo wa Uislamu mbeleni..

Tugeukie Ulaya katika uchunguzi wetu, tutashuhudia vyanzo vya habari vikikiri Uislamu utakuja kuwa dini itawalayo barani ulaya. Kutokana na *The Washington Quarterly*:

“...Waislam watafanikiwa kujumuisha sio chini ya asilimia 20 ya wana ulaya wote ifikapo mwaka 2050. Baadhi washaanza kutabiri kuwa robo ya Ufaransa itakuwa ni Waislam ifikapo mwaka 2025 na kama mwenendo huu utaendelea, Waislam watawapiku wasio-Waislamu kwa idadi huko Ufaransa na hata Ulaya Magharibi yote ifikapo 2050.”³⁵

Patrick Buchanan ni mchambuzi wa masuala ya kisiasa Marekani, mwandishi, mwanasiasa na vile vile ameshafanya kazi kama mshauri wa Rais (wa Marekani) Richard Nixon, Rais Gerald Ford, na Rais Ronald Reagan. Katika hotuba yake aliyoitoa tarehe 7 Desemba 2001, Buchanan alisema: “Msisahau kuuhesabu Uislamu, kwanza ndio imani inayokuwa kwa kasi zaidi barani Ulaya na pia imeshaupiku Ukatoliki duniani. Na kama tunavyoona Ukristo unavyokufa katika mataifa ya magharibi, makanisa yanazidi kupoteza watu na misikiti lukuki kuzaliwa na kujaa.”³⁶ Mwaka 1999, ukaguzi wa Umoja wa Mataifa ulionesha kuwa kati ya mwaka 1989 na 1998, idadi ya Waislam barani Ulaya imekuwa kwa asilimia zaidi ya mia moja.³⁷ Kwa sasa, Waislam

34. Taylor, Jerome. Morrison, Sarah. “The Islamification of Britain: record numbers embrace Muslim faith.” *The Independent* 4 Jan 2011. Also see: Brice, Kevin. A minority within a minority: A report on converts to Islam in the United Kingdom. Faith Matters, 2011.

35. Savage, Timothy M. “Europe and Islam: Crescent Waxing, Cultures Clashing.” *The Washington Quarterly* Summer 2004. p.28.

36. Buchanan, Patrick J. “Coming Clash of Civilizations? Theamericancause.org 7 Des 2001. <http://www.theamericancause.org/patcomingclashprint.htm>.

37. Allen Jr., John L. “Europe’s Muslims Worry Bishops.” *National Catholic Reporter* 22 Okt 1999.

wanawakilisha karibu asilimia 10 ya watu wa Ulaya yote na tabiri zinaonesha ifikapo mwaka 2025 Waislam watakuwa washafikia asilimia hizo (kumi).³⁸ Cha kufurahisha sasa! Amsterdam na Rotterdam ndio majiji yanayotazamiwa kuwa wakwanza kwa idadi kubwa ya Waislam ifikapo 2015 tu.³⁹ Katika makala iliyobeba kichwa cha habari “Ulaya, usimamaji wa magorofa marefu yanaakisi kuinuka kwa Uislam” iliongelewa katika *The Christian Science Monitor*, Isabelle de Pommereau anaeleza: “Ulaya, Uislam kama dini ikuayo kwa kasi zaidi kuliko zote unajijengea nafasi yake wazi wazi sasa baada ya milongo ya kuswali na kuabudu kwa kujifichaficha kwenye uga na sehemu za nyumba zilizo chini ya ardhi (basements), na sasa unafanikiwa sio tu kabadilisha sehemu zao za kijamii bali pia mandhari ya majiji.”⁴⁰ Akijadili mwelekeo wa kubadili mienendo ya dunia, William Van Wishard anatoa taswira akisema, “Kanisa Katoliki linakumbana na uwezekano mkubwa wa kufunikwa na Uislam kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi barani ulaya kwa miaka inayokuja.”⁴¹ Kuna sababu kubwa tatu zifanyazo bara la ulaya kuwa bara lenye Waislam wengi kuliko wafuasi wa dini nyengine, nazo ni 1) Uhamiaji 2) Kuzaliana sana kwa Waislam 3) Wanaosilimu.

38. “The Intergration of Muslims In Europe.” Oxford Analytica 24 Feb 2009. http://www.forbes.com/2009/01/23/france-uk-muslims-business_oxford.html last iliyopitiwa tena 29 Aprili 2009.

39. Pipes, Daniel. “Europe or Eurabia?” *Australian* 15 Aprili 2008.

40. Isabelle de Pommereau. “In Europe, skylines reflect the rise of Islam.” *The Christian Science Monitor* 26 Julai 2007.

41. Van Wishard, William. “Major Trends Reshaping The Global context.” Worldtrendresearch.com <http://www.worldtrendresearch.com/major-trends.php> baada ya kupitiwa tena 12/09/2009.

Hapa tunavutika na sababu ya tatu kwa kuwa ndio sababu inayotokea kwa haraka na wepesi zaidi. Utabiri maarufu wa Bernard Lewis* unasema bara la Ulaya litakuwa la Kiislam ifikapo mwisho mwa karne hii.⁴²

Mwaka 2005, *The Christian Science Monitor* lilisema: “Japokuwa hakuna takwimu za uhakika, ila kwa mchunguzi makini atagundua tu kuwa maelfu ya wanaume na wanawake wanasilimu mwaka hadi mwaka.”⁴³ Waislam waliokuwa Ulaya watawabadili wasio-Waislamu wa ulaya kuingia katika Uislam. Eidha Waislam watafanya jitihada kuzishinda roho za wasio-Waislam au watu wa bara la Ulaya wataasilimu kufuatia lile shauri la “Nimeamua kubadili dini kutokana na kuvutiwa na tabia njema na nidhamu ya Waislamu” au wanaweza kusilimu ili waweze funga ndoa na Muislamu. Au uwepo wa Waislamu nchi za Magharibi, kutachokonoa wasio Waislamu waweze kujifunza yaliyo katika mila ya Uislam na vipi waweze kuishi na Waislamu hawa wakali. Hivyo baadhi watatafuta vitabu kama *The Complete Idiot's Guide to Understanding Islam* cha Yahya Emerick kinachoweza kumsaidia asiye Muislam kujifunza misingi ya Uislam na kuishi nao. Vile vile, miongozo inayopatikana katika vitabu visivyowatisha kama *Islam For Dummies* pia vinaweza kuwasaidia wasio Waislamu kutambua misingi na masuala mengine ya Kiislamu. Wengine wanaweza kutumia vitabu vyengine vya kisomi zaidi vya Kiislamu na matokeo yake, wasio Waislamu watakuja kuuelewa Uislam halisi, ambao ni tofauti kabisa na ule unaofundishwa kupitia vyombo vya habari na mwishowe waukubali kwa kuingia ndani yake. Hapa tunapata ile kanuni ya ‘Uwepo-wako-unavuta-fikra-

* Profesa Bernard Lewis alipokea tuzo ya AEI's Irving Kristol mwaka 2007. Alifanya utabiri wake hapo juu mwaka 2004. Hundley, Tom. “Article of Faith for some: Europe Going Muslim.” *Chicago Tribune* 25 Juni 2006

42. Lewis, Bernard. “Europe and Islam”. *American Enterprise Institute*. 7 Machi 2007 (katika hafla ya chakula cha jioni ya AEI, alipofanya muhadhara Irving Kristol: Washington). Pia tazama Machils, David na Tovah Lazaroff. “Muslims about to take over Europe.” *The Jerusalem Post* 29 Jan 2007.

43. Ford, Peter. “Why European Women Are Turning to Islam.” *The Christian Science Monitor* 27 Des 2005.

zangu'. Pengine hii sababu ya tatu ndio iliyojumuishwa katika moja za hotuba za marehemu Gadhaifi: "Tuna Waislam wapatao milioni 50 barani Ulaya. Kuna kila dalili zioneshazwa Allah karibuni ataupatia ushindi Uislam katika bara hilo tena bila upanga, bila mtutu, na wala uvamizi. Waislam milioni 50 hao watabadilika kuwa bara la Kiislam miongo kadhaa baadae."⁴⁴

Ulaya, Uislam unashika nafasi ya pili kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi.⁴⁵ Kutokana na mazoea yetu maishani, mwanafunzi shuleni, kama kazoea kupata D anauwezo wa kupanda hadi C na halafu daraja la B. Na kama akiongeza juhudi na kujituma, bila shaka anao uwezo wa kufikia daraja la juu (A). Hivyo, katu haitashangaza kuona Uislam ukiusambaratisha Ukristo na dini zengine zote katika bara hilo la Ulaya. Kama Uislam ni dini ishikayo nafasi ya pili kwa sasa, bado ina nafasi ya kuwa dini itakayoshika nafasi ya kwanza hapo baadae. Katika mahojiano na balozi wa Sweeden nchini Uturuki; Ingmar Karlsson ambaye pia ni dokta wa kitaaluma katika masomo ya dini ya Kikristo katika Chuo Kikuu cha Lund. Pia ni dokta wa Falsafa katika Chuo Kikuu cha Vaxjo na ni mtunzi wa vitabu zaidi ya 10 ameelezea Uislam kama dini ya nyumbani Ulaya. Alisema katika mahojiano yake hayo: "Wakati nilipokuwa nakua kule Sweeden baada ya vita kuu ya pili ya dunia, kulikuwa na Waislam watatu tu nchini mwetu, watatu huwezi amini!... Sasa hivi Waislam wanawakilisha asillimia 5 mpaka 6 ya wananchi wa Sweeden wote. Na inavyoonesha hii idadi inakuwa siku hadi siku, naamini punde watu watakubaliana nami kuwa Uislam ndio na utakuwa ndio dini ya ulaya."⁴⁶ Pia alishangazwa na wale wasioona mabadiliko ya Uislam barani humo kwa kusema, "Eti watu bado hawajaujua Uislam! Inashangaza watu bado hawajangundua kuwa Uislam ndio dini ya ulaya..."⁴⁷ aliongeza

44. Edwards, Ruth Dudley. "Will Britain one day be Muslim?" *The Daily Mail* 5 Mei 2007. Pia tafuta kupitia [Al Jazeera Television](http://www.aljazeera.com). 10 aprili 2006.

45. Esposito, John L. "Introduction John L. Esposito." Katika historia ya Uislamu Oxford. Ed. John L. Esposito. Oxford [Islamic Studies Online](http://www.oxfordislamicstudies.com). 11 machi 2009. Pia angalia: "Observing Islam." [Online Newshour](http://www.pbs.org/newshour/bb/religion/july-dec01/islam_11-16.html). Pbs.org. 16 Nov.2001. http://www.pbs.org/newshour/bb/religion/july-dec01/islam_11-16.html

46. "Islam is and will be European religion" *Today's zaman* 12 Machi 2007.

47. "Islam is and will be European religion" *Today's zaman* 12 Machi 2007.

Kutoka kwa mwanahabari wa *Chicago Tribune* Evan Osnos ambae alisema: “Kwa Ulaya,...swala sio kipikitakachotawala kati ya umagharibi na Uislam, lakini lipi kati ya madhehebu mengi ya Uislam ndio yatakayo tawala.”⁴⁸ Wengine wanaweza wakachukulia yafuatayo kama dalili ya zao la Uislam kushinda barani Ulaya: Bara la Yuropa (Ulaya) litakuwa na misikiti na minara yake mingi kuliko makanisa na majengo mengine ya dini hiyo; *Adhiana*, wito kuwaita watu kufanya ibada ya swala, itavuma kutoka Paris mpaka Rotterdam, hadi Brussels na London; vijana wa Kiislamu wenye ndevu watafurika mitaani; Waislamu wawe viongozi wa nchi katika dola zote za bara hilo; Wakristo sasa wapiganie haki zao za wachache; uhuru wa kujieleza (freedom of expression) kiholelaholela uwe mashakani maana Shariah za Allah zitatawala; maduka ya nguo yanayouza nguo za kike yatakuwa hayakosi Niqaab (hijab ya kufunika uso), hijaab na nguo nyengine nzuri za Kiislamu; wanasesere waliovalishwa hijab nao kujaa masokoni kwa ajili ya watoto kuchezea; wafanyabiashara wanaopenda kuchunguza mahitajio ya wateja wao watashindana kufungua migahawa inayowapatia pizza halali; kuanzishwa kwa taasisi zinazowafikiana na Uislamu kama vyuo vikuu vya wanawake tu (na wala sio ule wa mchanganyiko baina ya wasichana na wanaume); wazungu kutoka Ulaya wengi wawe wazungumzaji Kiarabu kama lugha yao ya pili na pia lugha hiyo ya Kiarabu kufundishwa mashuleni; Madrasah (shule za kufundisha dini ya Kiislamu) za kisasa zitaenea kila kona ya mtaa...

Nzi Bilioni Moja Hawawezi Kuwa Makosani

Ukweli kuwa makundi kwa makundi ya wasio-Waislam kuingia kuukubali nakuingia katika Uislam hakuwezi bado kuthibitisha kama Uislam ndio dini ya kweli. Je tunatakiwa kuchukulia kinyesi kuwa ni mlo mzuri na wa kipekee eti kwa kuwa nzi bilioni hawawezi kuwa makosani?! Au yatupasa tumuamini yule muathirika wa uvutaji sigara ambaye kwa majigambo anatamba kwa kusema:

48. Osnos, Evan. “Islam shaping a new Europe.” *Chicago Tribune* 19 Des 2004

“uvutaji wa sigara ni jambo zuri kiafya kwani mamilion ya watu wanavuta” mwengine anaweza kuchekeka kwa kuamua kusema kuwa Ukristo ndio dini ya kweli kwa kuwa ndio yenye wafuasi wengi zaidi duniani, lakini kutokana na takwimu na kweli tulizoziona hapo mwanzo kuwa Uislam utakuja karibuni kuupiku Ukristo na hapo tena imaanishe Uislam ndio itakuwa dini ya kweli?! La hashu! Hata watu wangapi waingie katika dini fulani kitakachojalisha ni eidha upo au hamna ukweli utakaowavutia watu wengi. Kweli idadi ni jambo la msingi na kiuhalisia kuna usalama kupitia idadi hasahasa idadi kubwa ya watu kama hao ikawa inaunga mkono ukweli na sio kufata mkumbo wa kufanya kila jambo ambalo unaona watu wanalifanya. Hata hivyo, wengi kama sio wote wa wale waliosilimu walifanya uchunguzi wa kutokuwa na upendeleo kabla ya kuukubali Uislam. Sema kweli jambo hili la Uislam kukua hasahasa kupitia watu kusilimu linahitaji umakini wa fikra zetu na linamuhitaji yeyote yule anayemtambua Mwenyezi Mungu aungalie tena Uislam kwa jicho la moyoni bila upendeleo wowote.



Sehemu ya 1.2

Watu Waerevu na Machaguo Sahihi



“Ewe mvivu, mwendee chungu, zitafakari njia zake ukapate hekima” [Mithali 6:6] Pichani wadudu chungu wakiwa wanavutika na asali, kwa makundi wanaikimbilia. Katika Qur’an kuna sura nzima yenye aya zipatazo 93 izungumziayo mdudu chungu. Ni sura ya 27 katika Qur’an takatifu.



“Mwenye busara huwa na tabia ya kufanya mafikirio mwenyewe, mtu mjinga huwa mfataji maono ya watu tu.”

~ Methali ya Kichina

Baadhi ya Watu Waerevu Waliofanya Maamuzi Sahihi

Kwa muhtasari, kubainisha ukweli uliozagaa kuwa watu wamekuwa wakiuingia Uislam siku hadi siku, tutaangalia baadhi ya watu walioamua kukana imani zao kwa ajili ya Uislam baada ya ufatiliaji na utafiti wa muda katika mambo ya kiroho yenye kusadikika. Wafuatao ndio miongoni mwa waliogundua ukweli wa Uislam na wakaukumbatia. Hawa wanawakilisha ncha tu katika pande kubwa la barafu. Imegundulika kusilimu limekuwa ni jambo mashuhuri na la kisasa kulifanya. Hawa watu waliingia katika Uislam kwa njia rahisi tu ya kushahadia na kuzifanyia kazi shahada mbili hizi: **“Hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na Muhammad ni Mtume wake”**.

Murad Wilfried Hofmann



“Kwa kawaida mtu huwa haponi katika ajali kama hii, rafiki yangu! yawezekana wewe una agenda ya siri na Mungu”.

~ Maneno hayo yalisemwa na daktari aliyemfanyia operesheni ya kidevu na nyonga Wilfred Hofmann. Ilikuwa mnamo mwaka 1951 wakati alipopata ajali mbaya na kupoteza meno 19 na kubaki na mdomo ulio vurugika.

Alizaliwa kutoka familia ya Kikatoliki tarehe 6 Julai 1931 kule Aschaffenburg, Ujerumani. Alipitia chuo cha Union College cha New York (1950-51) akisomea elimu-jamii(sosiolojia) na kumaliza masomo yake Chuo Kikuu cha Munich, ambapo alitunukiwa udaktari wa maarifa ya Sheria mwaka 1957. Akawa msaidizi wa profesa katika mambo ya sheria, na pia akasoma tena sheria za Marekani katika shule ya sheria ya Harvard ambapo alipata shahada ya sheria(1960). Akawa mkurugenzi wa mawasiliano wa Umoja wa Nchi za Magharibi na Marekani (NATO) kule Brussels tokea mwaka 1983 mpaka 1987. Kuanzia mwaka 1961 mpaka 1994, alikuwa mjumbe wa mambo ya nje wa Ujerumani na mbobeaji katika masuala ya kujilinda kupitia nyuklia. Akateuliwa kuwa balozi wa Ujerumani nchini Algeria (1987-1990), na kuhamishiwa Morocco kuanzia 1990-1994. Wakati akifanya kazi zake maalum katika balozi ya Ujerumani huko Algiers, Murad alipata fursa ya kushuhudia mgogoro kati ya Ufaransa na jeshi la Algeria. Kilikuwa kitendo cha muda mrefu kilichojaa matukio na vituko vya kukumbukwa ikiwemo kukabiliwa na falsafa za Kiislam kikapelekea Hofmann kusilimu mwaka 1980. Kuelewa zaidi kuhusu kusilimu kwake na maisha yake, tafadhali



pitia kitabu chake chenye kurasa 240 *Journey to Islam, Diary of a German Diplomat* (1951-2000). Pia unaweza kupitia kitabu chake kingine kiitwacho *Journey to Makkah* [kina kurasa 192] ambapo pia ameelezea safari yake ya kiimani kuelekea Uislam.

Kwa kudokeza tu, Murad alifatilia kazi za wanafalsafa kama Wittgenstein, Pascal, Swinburn na Kant, kisha akafikia uamuzi wa kuamini kuwa kweli Mwenyezi Mungu yupo. Murad akawa ni mwenye kujiuliza vipi Mungu sasa anawasiliana na viumbe wake hivyo ikampelekea afatilie maandiko. Akapanga kufatilia maandiko ya Kikristo, Kiyahudii na ya Kiislam.

Hata hivyo, maisha yake kule uarabuni yalisaidia sana katika safari yake hii ya kiroho. Alishawahi kusema, “Nilishuhudia uvumilivu na uwezo wa watu wa Algeria kuwahi kurudi katika hali ya kawaida wanapokuwa katika matatizo makubwa, nidhamu yao katika mwezi wa Ramadhani, kujiamini kwao katika kushinda, vile vile ubinadamu wao uliozunguukwa na maovu ya dunia.” Akahisi ni dini ndio iliyowafanya hivyo, na hivyo kumpelekea kukisoma kitabu chao cha dini yaani Qur’an. “Sijawahi kuacha kusoma mpaka leo hii,” Anaeleza. Hakuna shaka Qur’an ilifanya kazi kubwa ya kumbadilisha kuingia katika Uislam. Na hili analithibitisha katika kitabu cha *Religion on the Rise* ambapo aliandika:



Murad as a guest speaker to The Oxford-Princeton International Conference “*Muslims in Europe post 9/11*”, geared towards assessing the impact of the 2001 Terror attacks on the Muslim communities in Europe.

“Kawaida ya watu kimagharibi wanafanya istihzai na chochote kinachohusishwa na muujiza. Tunajua kuendea Ukristo watu wanavutika na miujiza mingi lakini kwa upande wa Uislam, utavutika na muujiza mkubwa mmoja tu nayo ni hii Qur’an. Ni kitabu cha kushangaza ambacho msomaji yeyote atajisikia mpya kama kwa moyo mkunjufu akijihusisha nacho. Waingiao katika Uislam wanakutana

na changamoto ya kutafakari wao wenyewe pasipo mtu mwingine kufikri kwa ajili yao. Zaidi ya yote, Qur'an in-aonya wale wanaofata bila kuuliza kutoka kwa wazazi wao. Na kama Wolfgang von Goethe alivyoelezea suala hili kwa kusema, ili Waislam wajitambe na imani yao, yapasa uchunguze kwa makini chochote ulichopokea toka kwa mzazi wako. Kwa mantiki hii, hata mandhari iliyowazi ya misikiti itawavutia wengi wamagharibi.”

Moja ya hazina yake ya akili, ni kuwa Murad alikuwa na ufahamu mzuri wa historia na imani ya Kikristo. Alikuwa kugundua kuna tofauti kubwa kati ya kinachoaminiwa na muumini wa Kikristo na kile ambacho profesa anakifundisha chuo kikuu. Alishangazwa na imani ya kurithi ya kikanisa iliyotengenezwa na Paulo ukilinganisha na ile ya Yesu mwenyewe. “Huyu (Paulo) ambaye asilani hajawahi kukutana na Yesu amepandikiza imani na kubadilisha yale yaliyokuwa ya Yesu!” Anasisitiza Murad.

Katika kufupisha safari yake ya mabadiliko, Dkt. Murad anakubali:

“Nilianza kuuona Uislam kupitia macho yake yenyewe(Uislam), imani iliyokuwa haijapotoshwa, imani nzuri ya kuamini Mungu mmoja na atakayebaki kuwa mmoja, ambae hajazaa wala hajazaliwa, na ambae hafanani na chochote wala yeyote. Ukilinganisha na miungu ya kikabila, kimila, na utatu, Qur'an imenionesha mwono ambao uliokuwa rahisi kuonekana na kueleweka, ulio wazi na kihistoria wazo lilokuwa na nguvu zaidi, wa kumtukuza Mungu. Taarifa za kiasili za Qur'an, mafundisho yake yenye maadili mazuri zilinivutia kuwa ndio kitu bora na kizuri kama dhahabu. Hivyo hakukuwa na nafasi ya kunishawishi nisiamini ukweli wa utume wa Muhammad. Wale wanaouelewa uasili wa mwanadamu hawawezi kushindwa kuamini hekima isiyo na mwisho aliyopatiwa binadam kutoka kwa Mungu katika njia ya Qur'an.

Na baada ya kusilimu alisema yafuatayo:

“Ni kipindi sasa! Nahangaikia ukweli kupitia maneno machache na kwa muda mfupi, nimejaribu kuandika chini kwa njia na mfumo mzuri kabisa ukweli wote wa kifal-safa, ambao kwa upande wangu utachukuliwa bila shaka yoyote. Na katika juhudi hizi nikagundua kuwa lile wazo la kiagnostiki (asadikiye kuwa hatuna habari za Mungu wala hatuwezi kuzijua) kuwa ni ujinga na upumbavu. Kwa kawaida mtu hawezi kuepuka uamuzi wa kuamini, kwani wazo la vyote vilivyombele yetu vimeumbwa lineaoneka kuwa wazi kabisa, wala halina mashaka. Na hivyo bila shaka yoyote Uislam unaonekana kuwa ndio amani kuu katika kweli zote. Nimegundua bila hofu yoyote

baada ya hatua kwa hatua, kuhisi na kufikiri kuwa nimekuwa

Muislam bado kuna hatua moja nahitaji niifanye nayo ni kubadilika rasmi.

Na nashkuru leo nasimama hapa Muislam. Nimeshawasili.”

“... Ukilinganisha na miungu ya kikabila, kimila, na utatu, Quran imenionesha mwono ambao uliokuwa rahisi kuonekana na kueleweka, ulio wazi na kihistoria wazo lilokuwa na nguvu zaidi, wa kumtukuza Mungu.”

Baada ya kusilimu kwake, alielewa kwanini Mungu alimnusuru katika ajali ya mwaka 1951. Ajali iliyowashtusha watu na hata kupelekea kuvunjwa moyo kama hujafa. “Baada ya miaka 30, siki ile ile niliyosilimu ndio nikaelewa tafsiri ya mimi kunusurika kutoka katika ajali ile,” Alisema

Mwanzo alikubuhu katika unywaji wa mvinyo lakini sasa kwa adabu kabisa alikataa kuikaribia pombe aina yoyote. Wakati alipokuwa anahudhuria vikao vya mchana wa Ramdhan, siku zote ilionekana sahani tupu mbele yake. Hoffmann alikwenda kuhiji mwaka 1992 na ameshafanya umra (Hijja ndogo) sio chini ya mara saba. Na ilipofika elfu moja kenda mia na tisini na tano Murad alijiuzulu kutumikia taifa katika masuala hayo ya nje ya nchi ili apate fursa zaidi kwa ajili ya kutumikia dini yake.

Murad amekuwa mjumbe katika bodi ya wakurugenzi ya Chuo Kikuu cha Kiislam cha *Ibn Rushd* kilichopo Andalucia, Cordoba, Hispania; na pia amekuwa mjumbe katika *Academy of Islamic Civilization Research*, kule Amman, Hashimite Jordan; vile vile ni mjumbe wa kutumainiwa na mshauri wa baraza la Waislamu *Central Council of Muslims* huko Ujerumani. Hoffmann pia ni mmoja kati ya watia saina wa *A Common Word Between Us and You*, ambayo ni barua ya wazi kati ya wanazuoni wa Kiislamu kwa viongozi wa Kikristo, kuashiria amani na maelewano. Barua hiyo



Murad Wilfried Hofmann in Berlin

ni wito wa amani baina ya Waislamu na Wakristo inayojaribu kuwafanya waumini wa dini hizi kuishi na kufanya kazi katika hali ya kawaida na maelewano ikizingatia hasa hasa mambo mawili ya msingi: {1} Kumpenda Mungu {2} Kumpenda jirani yako. Vitabu alivyotunga ni kama *Journey to Makkah* (*Safari ya Makkah* kilichochapishwa mwaka 1998 chenye kurasa 192); *Islam 2000* (toleo la 3 lililotoka 2001 kikiwa kina kurasa 72); *Religion on the Rise: Islam in the 3rd Millenium* (*Uislam Katika Milenia ya Tatu* kilichochapishwa mwaka 2001, kikiwa na kurasa 248); *Journey to Islam, Diary of A German Diplomat, 1951-2000* (*Safari Kuuelekea Uislam, Historia ya Balozi wa Ujerumani* kina kurasa 240); *Islam: The Alternative* (*Uislam Kama Mbadala*, kurasa 168, na toleo la pili lilikuwa mwaka 1997). Ukiachilia kuandika vitabu kumi kuhusu Uislam, Murad amekuwa mwandishi makala katika majarida mbali mbali kama *Islamic Studies* la Islamabad, *American Journal for Islamic Studies* la Washington na *Encounters* la Uingereza. Pia ni mwandishi wa gazeti la Kiislam la Ujerumani. Mwaka 1996 alitembelea makao makuu ya jeshi la marekani, Pentagon ambapo alikutana



na Bodi ya Kikristo katika Vikosi vya Kijeshi (Armed Forces Chaplains Board, AFCB) kujadiliana nao kuhusu kitu kama hicho kwa ajili ya Waislam katika jeshi kwa baadae. Tuzo alizotunukiwa ni kama Federal Cross of Merit (aliyogaiwa na Raisi wa wakati huo wa Ujerumani Dokta Carl Carstens mwaka 1984); Kamanda wa Mpangilio Stahili huko Italia; tuzo ya mpangilio stahili katika sanaa na sayansi, daraja la kwanza, zote Misri.


BwanaHoffmann ana mtoto kutoka kwa marehemu mkewe wa mwanzo(Mmarekani). Baada ya kustaafu akachukua makazi mapya kwa mke wake mwengine wa kituruki huko Istanbul. Murad anasafiri mno barani Ulaya na Marekani ya kaskazini. Mtoto wake pia anafanya kazi katika balozi.

Njia ya Mawasiliano:

Anuani- Graurherindorfer mtaa. 23, D-53111 Bonn, Ujerumani
nukushi: +49 – 228 – 633. 578

Simu ya mkononi: +49 -171- 544. 7740

Barua pepe: Wilfried.a.hofmann@t-online.de



- Hofmann, Murad Wilfried. Journey to Islam, Diary of a German Diplomat (1951-2000). Leicester: The Islamic Foundation, 2001. [Paperback: 240 pages]; Hoffman, Murad Wilfried. Journey to Makkah. Amana Publications, 1998. [Paperback: 192 pages]; Hofmann, Murad Wilfried. Religion on The Rise: Islam in the Third Millennium. Maryland: Amana Publications, 2001.p. 188-189; Hoffman, Murad Wilfried. Islam: The Alternative. 2nd ed. Amana Corporation, 1997. [Paperback: 168 pages]; Hofmann, Murad Wilfried. "Islamic Renaissance in the West: An Interview with Murad Hoffman." By Hossam Tammam. IslamOnline.net. 15 Jan.2004 < <http://www.islamonline.net/english/ArtCulture/2004/01/article07.shtml#111>>; Hofmann, Murad Wilfried. "Dissecting our troubled world." by Abdullah Aliq. Arches (The bi-monthly Periodical of the Cordoba Foundation) Aug-Sept. 2006. Issue 03, p.3; Watanabe, Teresa. "U.S. Freedoms Give American Muslims Influence Beyond Their Numbers." Los Angeles Times 29 Dec. 2000.]

Yvonne Ridley

“Kila siku nikiamka huwa nilikuwa nikifikiri itakuwa siku yangu ya mwisho”

~ Yvonne Ridley.

Karibu na jiji la Jalalabad, mnamo mwaka 2001 wakati utawala wa Kiislam wa Taliban ulivyokuwa hatamuni. Hata kamera zilipigwa marufuku katika utawala huo. Taliban walikuwa washatangaza vita tukufu kwa yeyote mpinzani wao. Mwandishi habari wa Kiingereza akiwa amealia Burka huku akiendesha punda wake alikuwa tayari kuchukua jukumu zito la kisiri katika sehemu hii ya



Afghanistan iliyokuwa ikitawaliwa na Taliban. Alijiingiza katika nchi kinyemela, hakuwa na kitabu cha utambulisho wakati wa kusafiri (paspoti) wala viza. Alikuwa ni jasusi wa kimarekani? Hakuna ambae aliweza kusema na kugundua mpaka pale yasiyotegemewa yalipotokea. Kamera ambao alijitahidi kuificha kwa ustadi katika burka lake ilimondoka na kuonekana na askari wa kitaliban ambae hakuwa mbali nae. Akatumia siku sita katika makao makuu ya usalama wa taifa kule Jalalabad kabla ya kupelekwa katika (chuo cha mafunzo) gereza la Kabul ambapo



kitanda kilikuwa ndani ya selo chafu yenye kachumba kadogo kisicho na maji; fikra zake zilimtuma kufanya matayarisho ya mwili wake kwa ajili ya zana mbali mbali za mateso kama za umeme, bakora, na hata kupigwa mawe mpaka kufa.

Labda alifikiri anawazidi ujanja wataliban! Kwani Yvonne aliahidi kuisoma Qur'an kama ataachiwa huru. Kule kwao Uingereza, mmewe aliangua kilio kutwa kucha pindi tu aliposikia kuwa Yvonne yuko katika mikono ya wataliban....

“Taliban ni utawala wa siasa kali, nadhani watafikiri ameenda kule kwa ajili ya kupeleleza.” Alisema huyo mumewe.

Yvonne Ridley alizaliwa mwaka 1968 huko Stanley, County Durham, Uingereza. Alikulia makuzi ya Kiprotestanti katika kanisa la Uingereza. Alikuwa mwimbaji mzuri tu kanisani na pia mwalimu wa mafundisho kwa watoto kanisani katika kijiji chao hicho kilichopo kaskazini mwa nchi h i y o .

Baadae, akawa mwandishi wa habari katika gazeti la *Sunday Express*. Kwa miaka ipatayo kumi Yvonne amekuwa akifanya kazi katika magazeti mbalimbali yenye hadhi kama vile *The Sunday Times*, *The Observer*, *Daily Mirror* na *Independent*.

**“Nikawa mbaya
kwa walioniteka,
niliwatemea mate,
mkaidi na nikagoma
kula.”**

Mwanahabari huyo ambaye alishawahi kupata tuzo, pia amefanya kazi kama mrusha matangazo, prodyuza na pia mtangazaji katika vipindi na mashirika tofauti kama BBC TV na redio, CNN, ITN na Chalton TV akisafiri sana Afghanistan, Iraq na Palestina.

Tukirudi katika tukio lake akiwa mikononi mwa Wataliban, Yvonne Ridley akaanza kuwa mkaidi. “Nikawa mbaya kwa walioniteka, niliwatemea mate, mkaidi na nikagoma kula. Sema kweli sikuvutiwa na Uislam hata kidogo mpaka pale nilipokuwa huru kutoka katika mikono hii.” Alisema. Mmoja kati ya wale waliomteka alimuomba awe Muislam akakataa, lakini hata hivyo akaahidi kama akiachwa huru ataisoma Qur’an. “Nilitoa ahadi kwa sheikh wakitaleban kuwa nitausoma Uislam kama nikiachiwa. Nilisema hayo baada ya kuulizwa kuhusu utayari wangu katika kuukubali Uislam na nikahofia kutoa jibu la ‘ndio’ au la ‘hapana’ kwani iliwezekana majibu yote yakaeleweka vibaya na kutafutiwa sababu tu ya kupigwa mawe na kufa.” Siku kadhaa baadae Yvonne aliachwa huru bila kuumizwa kwa amri ya Mullah Omar, kiongozi wa kiimani wa Taliban ambaye ni mwenye jicho moja.



Kuhusu elimu na imani yake ya awali kuhusu Uislam, Ridley alisema “Sijui kitu kwani hata nikielezea nijuayo sidhani kama naweza jaza kile kikaratasi cha stempu. Ila ningeweza kuelezea yale yote yaitwayo maovu na ubaya wa Uislam kama unyanyasaji wa kijinsia, vipi ilivyo dini chafu na mbaya iliyojaa siasa kali.” Lakini baada ya kuisoma Qur’an ‘katiba impayo haki mwanamke (magna carta for women)’ kama alivyoiita mwenyewe, Yvonne akaamua kusilimu mwaka 2003 katika majira ya joto, ikiwa ni miaka miwili na nusu tu baada ya kukamatwa kwake. Aliacha vileo mwaka mmoja kabla ya kusilimu. Na kwa kweli huwa anajisikia fahari sana pale asikiapo mtu wa kwanza kusilimu alikuwa ni mwanamke naye ni mke wa Mtume (Khadijah bint Khuwailid) na asikiapo kuwa shahidi (aliyekufa kwa ajili ya dini) wa kwanza pia alikuwa ni mwanamke (Sumayya). Yvonne anapenda kuvaa hijab. “Inaieleza dunia kuwa mimi sasa ni Muislam: usinipige, usiniongeleshe ovyo, usinialike katika vilevi wala nyama ya nguruwe; na kama ukihita tuzungumze yatupasa kuzungumza mambo ya msingi tu. Na mpaka sasa sikumbuki lini ilikuwa siku

ya mwisho mtu kunitania utani mchafu, napenda waendeleo hivyo....” Alisema.

Akishangazwa na ukweli wa Qur'an, alisema, “Niliathirika sana na nilichokuwa nakisoma- hakuna hata kanukta kalichobadilishwa (katika Qur'an) kwa miaka zaidi ya 1400 sasa.” Akilinganisha haki za wanawake kutoka katika Qur'an na zile wanazojiita haki kule Magharibi, Ridley alinena, “Kitu cha kwanza kukifatilia katika Qur'an kilikuwa ni sheria za ndoa, talaka na mali. Nikashangazwa sana. Nilikikiri (Qur'an) imeandikwa na wakili wa sheria kutoka Hollywood (eneo Marekani maarufu na mahsusi kwa ajili ya matengenezo ya filamu). Kwa kweli, ni kutoka humu ndio wamepata wanayoyadai.” Katika kutimiza ahadi yake aliyotoa kule gerezani, ilimbidi apate kazi ya kuzunguuka kwa wanazuoni mbali mbali waaminikio wa Kiislam kwa ajili ya utafiti zaidi wa Uislam. Alikwenda kwa dokta Zaki Badawi kwa ajili ya ushauri na ufafanuzi; akagaiwa vitabu vingi vya sheikh maarufu Abu Hamza Al-Masri ambae alionana nae baada ya wote kuhutubia katika majadiliano (debate) ya pamoja kule Oxford.

Pia ameweza kumsikiliza na kuonana nae Dkt. Muhammad Al-Massari, kumuelezea masuala kadhaa ya Uislam. Kuusoma kwake Uislam kulipelekea kuja kusema haya:

“Hii Qur'an imeweza kuandikwa jana kwa ajili ya leo. Inaweza kukaa pamoja na mwanaharakati yeyote wa mazingira, ni rafiki mzuri wa mazingira na ni wazo kuu kwa ajili ya karne hii ya 21, chakushangaza haijabadilika hata neno moja tangu iandikwe sio kama haya matabu mengine makubwa na mazito yanayotazamiwa kuja kuleta tija.”

Badiliko lake lilikumbana na mitihani na vikwazo vigumu, yote ni tu kwa kuwa ameamua kuwa muumini mzuri wa Uislam avaaeye hijab. Kulikuwa na dereva wa taxi aliyesema, “Usiache bomu katika siti ya nyuma” na kuuliza, “Wapi ambapo Bin Laden amejificha?”

Ridley ameandika kitabu kilichobeba jina la *In the Hands of Taliban* (*Mikononi Mwa Wataliban*) kilichochapishwa na Robson Books huko Uingereza. Kitabu kingine alichotunga ni *Ticket to Paradise* (*Tiketi Kuelekea Peponi*). Baada ya kusilimu tu Ridley alienda kuhiji. akieleza yaliomsibu akiwa anahiji, Ridley alisema:

“Hija ni zoezi zuri na la kushangaza. Kwa yeyote ambaye bado hajabahatika kuhiji namuusia afanye hivyo upesi. Inakuonesha mizizi ya Uislam. Kwangu mimi jambo hili si la kusahaulika kamwe. Siku moja nilikuwa naharakisha kuwahi jamaa (swala kwa pamoja na waumini wengine) ya swala. Nikiwa napita katika mitaa yenye kona nyingi kuelekea Haraam (msikiti mtukufu wa Makkah). Walikuwa malaki kama mie tukiwahi kuelekea swala. Ikawa vurugu njiani kwa kweli- kwani kila mtu alikuwa akisukuma sukuma ili aharakishe kufika katika Haraam kwa muda. Ghafla pakaqimiwa kuwataarifu watu wawe tayari kwa swala, kila mtu alisimama na bila zogo watu wote wakajipanga katika mistari haraka. Nikaanza kufikiria hakuna jeshi lolote duniani lenye uwezo wa kujipanga vile kwa haraka. Na hivyo nikabaki nafikiria jeshi la Allah tu na moyo wangu ukitabasamu kwa mimi kuwepo ndani yake. Macho yangu huwa yanajawa na machozi kwa kufikiri hili nililoshuhudia. Ilinifanya nifurahi kuwepo katika familia hii kubwa. Pale, kulikuwa na watu kutoka mataifa tofauti, lugha tofauti na rangi tofauti. Swala ikaanza, wote tulielewa na wote tuliungana katika muungano mzuri usio na fujo, zogo wala kelele. Ilinihuzunisha sana kugundua kuwa tutadumu vile kwa sekunde kadhaa tu, nikajjuliza kwani ni tusiendelee Waislamu kuwa hivyo baada ya swala pia!”

Yvonne ni mwanzilishi wa *Women in Journalism* (*Wanawake Wanahabari*), promota wa haki za wanawake na pia ni mwanzilishi wa *Stop the War Coalition* (*Muungano wa Vyama Kupinga Vita*) na chama cha siasa cha RESPECT. Pia ni mjumbe katika umoja wa wanahabari wa taifa *The National Union of Journalists*, *The International Federation of Journalists* (Shirikisho la Wanahabari la Kimataifa) na *The Society of Authors* (Umoja wa Waandishi, Watunzi). Kwa sasa, anafanya kazi kama mtangazaji katika kituo

cha televisheni kipatikanacho dunia nzima cha PRESS TV. Pia ni mwandishi katika kijarida cha kila siku chenye makao yake New York kiitwacho *Daily Muslims*. Kwa maneno yake mwenyewe akiongelea kuhusu kusilimu kwake, Ridley anajisifu kwa kusema “Nimejiunga na familia ambayo kwangu mimi naichukulia kama ndio kubwa zaidi kwa sasa duniani bila kusahau ndio familia bora zaidi pia. Kama tukishikamana basi hakuna wa kutuzuia.” Baadhi ya masomo yake yapatikanayo kutoka katika intaneti ni kama ‘*Conversion to Islam*’ na ‘*Journey to Islam*’.



Kuonesha kuumizwa kwake na haya mashambulizi ya kila siku katika kuusema vibaya Uislam, ameandika:

“...Kwa sasa inauma na kuchosha kuona hapa Uingereza Jack Straw (aliyewahi kuwa waziri wa mambo ya nje) akiielezea niqab (kujifunika uso kasoro macho tu) kama ni kikwazo kikubwa cha muingiliano katika jamii na hapo hapo waziri mkuu Tony Blair, mwandishi Salman rushdie na waziri mkuu wa Italia Romano Prodi wakiwa upande wake. Nikiwa nimepitia pande zote mbili, nakwambieni, wengi wa wanasiasa na wanahabari wakimagharibi ambao wanaonesha



kuchukizwa na unyanyasaji wa wanawake katika maeneo ya Waislam hawajui walisemalo. Wanaongelea kujifunika, ndoa za watoto, ukeketaji wa wanawake, mauaji matukufu, na ndoa za kulazimishwa na wanaanza kuulaumu Uislam kimakosa. Jeuri yao imezidiwa na ujinga wao. Hizi tamaduni na desturi za watu hazihusiani Abadan na Uislam. Ukiisoma Qur'an kwa makini utagundua kuwa kila kitu ambacho hao wajiitao wanaharakati katika nchi za magharibi wanakipigania kilikuwepo kwa Waislam wanawake miaka 1400 iliyopita. Wanawake katika Uislam wako katika daraja moja na wanaume katika ucha Mungu, elimu na umilikiji mali. Na hii zawadi ya mwanamke kuzaa mtoto na kumlea tunalichukulia kama ni ushindi kwetu. Wakati Uislam unamgaia kila kitu mwanamke kwanini wanaume wa kimagharibi wapoteze muda wao kufatilia mavazi ya mwanamke wa Kiislam!? Hata mawaziri kama Gordon Brown na John Reid wamevalia njuga kuzungumzia niqab na wanatupia mbali yale yatokeayo hapo mpakani tu mwa Scotland (Uskochi) kwa wanaume kuvaa sketi....kipi ndio chafaa kutazamwa zaidi, kuhukumiwa kwa kuvaa sketi ndefu na umbo la matiti yako uliyoyarekebisha kwa operesheni au kuhukumiwa kwa kuangalia akili na tabia za mtu? Katika Uislam ubora unapatikana katika uchaji Mungu pekee, sio katika uzuri, mali, nguvu, cheo, au jinsia. Sikujua kama nilie au nicheke wakati waziri wa Italia; Prodi, alipoingilia majadiliano (debate) wiki iliyopita na kutangaza eti ni jambo la kawaida tu mtu kutovaa niqab kwani inafanya maingiliano katika jamii magumu. Huu kusema kweli ni upuuzi! Kama ni hivyo kwanini basi simu, barua pepe, ujumbe mfupi wa maneno, na nukushi vinatumika kila siku? Na huwezi ukakuta mtu anazima redio eti kwa sababu hamuoni mtangazaji.



Njia ya Mawasiliano:Tovuti: www.yvonneridley.orgBarua pepe: hermosh@aol.com

Simu: 078 36 370 649

Anuani:

1b Silver place

London

W1F 0JW, ENGLAND

references

[Blair, Tom, and Paul Stokes. "British journalist is seized by Taliban." Telegraph 29 Sep 2001; Bayman, Hannah. "Yvonne Ridley: From captive to convert." BBC News Online 21 Sept. 2004; Ridley, Yvonne. "How I Came To Love The Veil." Washington Post. 23 Oct. 2006; Napier, Eloise. "Articles of Faith." The Guardian, 24 Feb. 2004; Childs, Roger. "A Muslim in the family." bbc.co.uk <<http://news.bbc.co.uk/1/hi/programmes/3663771.stm>>; Rachel Cooke "Free radical" The Observer. 6 July. 2008; "Yvonne Ridley." Inside Out. BBC 6 Oct. 2003. <http://www.bbc.co.uk/insideout/northeast/series4/yvonne_ridley_iraq.shtml>; "Yvonne Ridley, Taliban Captive and Soon-To-Be Muslim, Speaks to IslamOnline." by Mohammed Ayub Khan. Islamonline.net 27 Aug. 2002 <<http://www.islamonline.net/English/Views/2002/08/article12.shtml>>; Ridley, Yvonne. "My Journey to Islam." The Muslim News 30 Aug. 2002; Ridley, Yvonne. "My Journey to Islam." Q-News 5 March. 2003; "Yvonne Ridley." cbc.ca <<http://www.cbc.ca/thehour/videos.html?id=739052643>>]

Jeffrey Lang

“Mungu atakufanya umpigie magoti, Jeffrey!”

~ Hayo yalisemwa na baba yake kutokana na Jeffrey kubisha uwepo wa Mungu akiwa na miaka 18.



Dkt. Jeffrey Lang aliyezaliwa 30 Jan 1954 huko Bridgeport, Connecticut ni Profesa mkuu wa hisabati katika Chuo Kikuu cha Kansas, moja ya vyuo vikuu vikubwa Marekani. Lang alizaliwa katika familia ya Kikatoliki. Japokuwa alienda

katika shule ya Kikatoliki alipokuwa na umri wa miaka 16, Jeffrey alikuwa mpagani. Kupitia kote shahada yake ya kwanza, ya pili na ya tatu bado Jeffrey alibaki mpagani akiwa haamini Mungu kabisa. Akaamini na kuingia katika Uislam mapema miaka ya 1980. Jeffrey alipokea Ph.D. (udokta kitaaluma baada ya kupata shahada tatu na zaidi) yake kutoka Chuo Kikuu cha Purdue mwaka 1981. Tasnifu (thesis) yake chuoni ilikuwa kuhusu *Zariski surfaces* aliyoandika chini ya usimamizi wa William Heinzer na Piotr Blass. Maandiko yake marefu ya mada yanayohudhurishwa kwa digrii ya chuo kikuu (dissertation) yalipewa kichwa: *The Divisor Classes of The Surface $Z_{p^n} = G(x, y)$ Over Fields Of Characteristic $P > 0$* . Lang alipendelea Algebra katika tafti zake.

Kuwa pamoja na mwanafunzi wake, ambae ni Muislamu mwenye asili ya Uarabuni kumempelekea na yeye kuwa muislam. Lang

**“Hesabu hutumia
akili. Inajumuisha utumizi wa
ukweli na maumbo kupata majibu
sahihi na ya wazi kabisa. Na hivyo
ndivyo nilivyouzo esha ubongo wangu.
Huwa inavunja moyo kama niki-
ushughulisha na vitu ambavyo
havina majibu sahihi
na ya wazi”**

na ya
ndivyo nilivyouzo esha ubongo wangu. Huwa inavunja moyo
kama nikiushughulisha na vitu ambavyo havina majibu sahihi
na ya wazi”. Tabia hii ilimfanya asivutike na imani ya upofu
itlewayo na dini nyingi.

alisema, amekuwa
s i k u z o t e
anavutiwa na
hisabati kwa
s a b a b u ,
“hesabu
hutumia
a k i l i .

Inajumuisha
utumizi wa
ukweli na maumbo
kupata majibu sahihi
wazi kabisa. Na hivyo



Dkt. Jeffrey Lang ni Profesa wa hisabati katika chuo kikuu, na ni Muislamu



Mwanzoni mwa mapitio yake Qur'an, Dkt. Lang alifurahishwa sana hadi ikafikia kukiri kwa kusema:

“Wachoraji au wapigaji rangi wanaweza kutengeneza macho ya mchoro wao yakawa yanakufata kila mahali utapokuwa unahamia, lakini mtunzi gani anaeweza kuandika maandiko yanayofatilia maisha yako yote ya kila siku? ...kila usiku nilikuwa natengeneza maswali na kesho yake asubuhi navumbua jibu (katika Qur'an). Inaonekana kuwa mwandishi wa kitabu hiki alikuwa anafatilia mawazo na maisha yangu na kuandika -katika mistari iliyopangiliwa kwa ustadi na uhodari wa aina yake- majibu yote yaniumizayo kichwa ili niyaone nikisoma tena. Kwa kweli nimejikuta mwenyewe humo katika kurasa hizo....”

Pia alisema,

“Huiwezi kuisoma (Qur'an) kirahisirahisi tu, ni eidha utajisalimisha kwayo au kuwa mpingaji kwake. Inakushambulia bila kuchoka, tena moja kwa moja na mahsusi kwako; inajadili, inaponda, inaumbua na inakuhoji. Tokea mwanzo, inachora mstari wa mapambano na mimi nikiwa upande wa pili....kwa wale ambao wameukubali Uislam sasa, shahidi wao mkubwa kuonesha upendo wa Mungu kwao ni hii Qur'an. Kama bahari kubwa yenye kuvutia, huwa inavutia uende zaidi na zaidi mpaka unajikuta ushazamishwa kwa mawimbi yake. Lakini kinyume na hapo juu, ambapo unazamishwa katika giza, hapa utajikuta umezama katika bahari yenye nuru na rehema.... wakati nilivyokuwa nikisoma Qur'an na kuswali swala za Kiislamu, mlango wa moyo wangu ukabikiriwa na nikazamishwa katika bahari ya hisia tofauti. Upendo ukawa wa kudumu na halisi kuliko hata ardhi chini ya nyayo zangu. Nilikuwa mwenye furaha kuonja imani kupitia dini iliyowazi yenye kueleweka. Kwa kweli sikuwa nafikiria kama nitaguswa na 'sumu' hizi za rehema ya Mungu.”

Yeye ni mtunzi wa vitabu vyenye mauzo makubwa : *'Struggling to Surrender'* (Jitihada za Kujisalimisha) na *'Even Angels Ask: A Journey to Islam in America'* (Hata Malaika Wanauliza: Safari Kuuelekea Uislam Marekani). Kitabu chake kipya zaidi ni *'Loosing My Religion: A Call For Help'* (Kuiacha Dini Yangu: Wito Kwenye Msaada). Ukiachana na makala na vitabu vingi alivyoandika, Lang amekuwa mualikwa katika hafla tofauti ili ahutubie. Baadhi ya hotuba zake ni :

- ▶ The Purpose of Life (Dhumuni la Maisha - video)
- ▶ Winning Our Children Back to Islam (Kuwavuta Watoto Wetu Waurejee Uislam - video)
- ▶ Men and Women's Relations in Islam (Uhusiano wa Mwaname na Mwanamke Katika Uislam - kipindi katika televisheni)
- ▶ Qur'an and My Life: A Guidance and Light (Qur'an na Maisha Yangu: Mwongozo na Nuru)
- ▶ Understanding Islam: The Qur'an (Katika Kuuelewa Uislam)
- ▶ Pillars of Islam: The Spiritual Dimensions (Nguzo za Uislam)
- ▶ Islam Between Faith and Reason (Uislam Kati ya Imani na Utumizi wa Akili)




Lang kamuoa mwanamke Muislam kutoka Saudi Arabia aitwae Rakia na wamebahatika kupata watoto watatu; Jameelah, Sarah na Fattin. Unaweza kumuona Lang akielezea sehemu ya maisha yake kupitia

<<http://www.youtubeislam.com/video/1857/>

DrJeffrey-Lang-at-the-DeenShow>

<<http://www.youtube.com/watch?v=iflgTA2pmY&feature=relmfu>>

Unaweza pia kununu video zake kama “The Purpose of Life” kutoka <<http://www.onlineislamicstore.com/a3851.html>>



Jeffrey Lang akitoa hotuba iitwayo “Dhumuni la Maisha”



Njia ya Mawasiliano:

The University of Kansas

Department of mathematics

Ofisi: 509 Snow Hall

Simu: (785) 864-3055

Nukushi: (785) 864-5255

Barua pepe: lang@math.ku.edu

Tovuti: <http://www.math.ku.edu/~lang/>



references

[Lang, Jeffrey. Losing My Religion: A Call For Help. Amana, 2004. (Paperback: 512 pages); Lang, Jeffrey. Struggling to Surrender: Some Impressions of an American Convert to Islam. 2nd ed. Amana Publications, 2000. (Paperback: 242 pages); Lang, Jeffrey. Even Angels Ask: A Journey to Islam in America. 1st ed. Amana Publications, 1997. (Paperback: 248 pages);

University Of Kansas Faculty Page <<http://www.math.ku.edu/people/faculty/jeffrey-lang.html>>; Jeffrey Lang at the Mathematics Genealogy Project <<http://www.genealogy.ams.org/id.php?id=16886>>; William Heinzer PH.D. Students, www.math.purdue.edu/~heinzerv/curr-vitae/students.html>]

Khadijah ‘Sue’ Watson

“Waislamu ndio watu wagumu zaidi kuihama dini yao’.

~ Haya yalisemwa na Mary Sue Malvar, mchungaji rasmi na mmishenari wa Kikristo.



Mary Sue Malvar ni Mmarekani kutokea California (Kalifonia). Ana shahada ya masomo ya dini (theolojia) na shahada ya pili akisomea Biblia mwaka 1993. Alikuwa ni mchungaji anaeaminika, aliyepewa mamlaka ya kufundisha ambae alitumia miaka saba kuhubiri dini huko Ufilipino. Mary, ambae ni profesa wa theolojia, alihamia kutoka katika

Ukatoliki kwenda kweye ulokole. Alivyokuwa kazini kwake huko alimaanisha kweli kile alichokisema “Waislamu ndio watu wagumu zaidi kuihama dini yao. Na hii ni kwa sababu hakuna jipya unaloweza kuwapa kwani katika uislam kuna uhusiano mzuri na Mungu, kusamehewa dhambi, kuokoka na ahadi ya kwenda peponi”.

Kukutana kwake na mmoja kati ya waliosilimu kulimfanya naye kufanya upekuzi ya kutaka kugundua kunani katika uislam na mwishowe kukiri kuwa “Wakristo wengi wako kidhati ila cha kusikitisha wapo katika uongo wa dhati.” Baada ya kuamua kuusoma uislam kutoka katika vyanzo vyake, katika kipindi cha wiki moja, alikuwa ameshakamilisha vitabu 12 na akawa ametumia masaa yasiopungua 15 katika mijadala mbali mbali ya dini. “Nilijua tu kama uislam ni ukweli,” Aliyasema hayo baada ya uchambuzi



**"Nilijua tu
kama Uislam
ni ukweli"**

wake wa dini. Kwa kusoma zaidi na dua zake ili aongozwe, Mary aliamua kuwa muislam na kubadili jina lake kuwa Khadijah Sue Watson. Mmoja wa watoto wake aliwahi kunukuliwa akisema, "Mama, amekuwa mtu mzuri zaidi sasa kuliko alivyokuwa mwanzol!" na hili lilimshangaza kama alivyosema "...wakati nikiwa Mkristo, nilijaribu kukiweka kimatendo kila nilichoamini".

'Sue' Watson ambae alikuwa mchungaji na professa wa Biblia akafikwa na wakati mgumu pindi tu alivyosilimu. Ndio maana hapa akasema:

"Nilifukuzwa kazi yangu nikiwa kama mwalimu katika vyuo viwili vya Biblia kwa wakati mmoja, nikatengwa na niliosoma nao, maprofesa, wachungaji na mapadri, kutengwa na familia ya mume wangu, kutoeleweka kwa watoto wangu wakubwa na kuanza kuhisiwa vibaya na serikali yangu. Bila ya imani inayoweza kumkinga mtu kutoka katika nguvu za sheitan nisingeweza kuvivumilia hivi vyote. Nafurahi sana kwa Allah kuwa muislam na namuomba Mungu niishi na kufa nikiwa muislam. "...Hakika Swala yangu, na ibada zangu (zote nyengine) na uzima wangu, na kufa kwangu; (zote) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Muumba wa walimwengu wote. (Likinisisibu jambo limenisibu kwa kutaka Mwenyezi Mungu si kwa kutaka viumbe Vyake. Na yote ninayoyafanya nayafanya kwa ajili Yake.) "Hana mshirika. Na haya ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu.)" [Q 6:162-163]

Khadijah Watson kwa sasa, anafanya kazi ya ualimu pale Al-Hamra Islamic Education Foundation kule Jiddah, Saudia Arabia. Mmoja kati ya watoto wake tisa amebadili dini na kuwa muislam baada ya kusoma vitabu vya kiislam vya mama yake kisirisiri.



Njia ya Mawasiliano:

Tovuti: www.islamuncovered.com



[Muslim World League Journal; Danial bin Zainal Abidin. Islam: The Misunderstood Religion. PTS Millennia: 2005. p.112; <<http://thetruereligion.org/modules/xfsection/article.php?articleid=244>>]

Cat Stevens

“Ewe Mungu! Kama ukiniokoa nitafanya kazi kwa ajili yako.”

~ Hapo Cat Stevens alipokuwa bichi (ufukoni) ya Malibu ambapo kuogelea kwake kwa starehe kulivyogeuka kuwa jinamizi. Alikuwa akihangaika kujinasua kuzama.



Ilikiwa mnamo terehe 21 Julai 1948, Steven Demtre Georgiou ambae baadae alijulikana sana kwa jina lake la stejini Cat Stevens alizaliwa tena kutoka kwa baba muumini wa kanisa la Kigiriki na mama muumini wa kanisa la Kisweden. “Nimezaliwa katika familia ya Kikristo ambayo iliheshimu pesa



na mie nikaingia katika mkumbo huo. Niliwapenda sana waimbaji (wanamuziki) ikafikia hatua wakawa ndio kama miungu yangu, baadae nikaamua kuwa mmoja wao. Nikaishia kuwa msanii

mkubwa wa nyimbo za pop, vyombo vya habari vikanifanya niwe supastaa mkubwa kuliko maisha yenyewe na hata nikaona kuwa mimi ni mtu wa kuishi milele,” Alisema.



Cat Stevens ni muimbaji, mtunzi wa nyimbo, mpigaji vyombo tofauti vya muziki, mkufunzi, na msaidizi wa watu wengi kimuziki na kimaisha. Amekuwa msanii mkubwa wa pop tangia ujana wake (kabla ya miaka 20). Kupitia jina lake la Cat Stevens amewahi

uza nakala za albamu zisizopungua milioni 60 duniani kote tangia miaka ya 1960. Msanii huyu maarufu anayetokea Uingereza alikuwa na uwezo wa kuingiza zaidi dola 150 000 kwa usiku mmoja ‘mfukoni mwake’. Cat Stevens alikuwa kashafanikiwa kupata kila kitu ambacho wengi duniani wanaota kuwa navyo: umaarufu, kipaji, utajiri, muonekano mzuri, na usumaku kwa jinsia ya pili, lakini bado akahisi kuna kitu anakosa. Japo kuishi kwake kote katika maisha ya ‘usupastaa’, Cat Stevens kwa mara moja ilitokea akapokea wito kutoka katika mwamsho wa kiroho. Alikuwa mgonjwa sana, akisumbuliwa na kifua kikuu na moyo. Hatimaye, Cat Stevens alilazwa hospitali kwa muda mrefu, jambo ambalo likamfanya atafute maana halisi ya kuishi.

Na ilipofika mwaka 1976, Stevens alipokea simu nyengine ya mwamsho wa kiroho. Na sasa, ilikuwa katika pwani ya Malibu huko California, ambapo alikuwa nusra afe maji kwa kuzama. Akapiga kelele sana “Ewe, Mungu kama ukiniokoa hapa, nitafanya kazi kwa ajili yako.” Na baada ya kuokoka pale, kweli alianza safari yake ndeefu ya kutafuta ukweli wa kiroho.



Alitazama katika imani tofauti tofauti kama vile Ubudha, Zen, I Ching, Numerolojia (imani ya nguvu kupitia idadi), na Astrolojia (uhusiano wa binaadam na mfumo wa jua). Baadae akaandika,

“Utafiti wangu wa muda mrefu uliendelea pamoja na muziki wangu mpaka siku rafiki yangu aliporudi toka Mashariki ya Kati na kunambia amepata utulivu toka msikitini ambao hakuweza kuupata alivyokuwa kanisani, na kunivutia kufatilia jambo hilo. Haraka haraka nikanunua Qur’an iliyotafsiriwa. Na kweli hatimaye nikapata majibu ya maswali yangu: Mimi ni nani? Wapi natokea? Na lipi ni dhumuni langu hapa duniani? Na baada ya kuendelea kupitia kitabu hiki nikagundua kweli kuna Mungu mmoja tu ambae tunaweza kuwasiliana nae pasipo na pazia lolote katikati.”

Ilikuwa ni Qur’an ndio iliyompa amani ya moyo aliyokuwa akihangaika kuitafuta siku zote. “...Naomba niweke wazi kuwa sikukutana na Muislamu yeyote kabla ya kusilimu kwangu. Nimeisoma Qur’an tu na nikaelewa hakuna mtu mkamilifu. Ila Uislam umekamilika na kama tukaiga mwenendo wa huyu Mtume aliyebarikiwa (rehma na amani ziwe juu yake) tutafanikiwa”.

Akaja kuelezea zaidi:

“Kila kitu chake kinaingia akilini. Na huu ndio uzuri wa Qur’an; inakufanya wewe utafakari na utumie bongo lako.... Wakati nilipoisoma Qur’an zaidi na zaidi, niliona ikiongelea kuhusu kusimamisha swala, huruma na sadaka. Nilikuwa bado sio Muislamu lakini nilihisi jibu la maswali yangu ni Qur’an tu ambayo Mungu atakuwa kaniletea zawadi.”

Akaingia rasmi katika uislam mwaka 1977, na kubadili jina kuwa Yusuf Islam mwaka 1978. Baada ya kusilimu, Yusuf Islam alitangaza kuwa muziki wake wa pop wote ulikuwa sio wa kiislamu, hivyo akapiga mnada magita yake, na rikodi zake zote na yaliyopatikana yote aliyatumia kutoa misaada ya kiislamu. Ilifika hatua hadi akalumbana na kampuni za muziki kuwa waache

kuhifadhi miziki yake ambayo mwenyewe alichukulia baadhi yake iko nje ya maadili. Kuelezea hitajio lake la kuuacha muziki alisema, "...nina ajenda nyengine ya kutimiza; nahitaji kuisoma imani yangu, kuangalia familia na kupangilia na kuziweka wazi vipaumbele vyangu."

Kwa makadirio Januari 2007, alikuwa bado anaingiza karibia dola za kimarekani milioni moja na nusu kwa mwaka kutoka katika muziki wake wa kale (Cat Stevens music), aliamua kutumia yale makusanyo ya maingizo yake yote katika kusaidia watu mbali mbali kimaisha na kielimu katika sehemu wanazopatikana Waislamu wengi kule London na kwengineko kama mayatima Bosnia. Mwaka 1982, yeye na Waislamu wenzake waliguswa kuona watoto wao hawapati elimu bora ya kiislamu kule kwao Uingereza. Hivyo, wakaamua kuanzisha Mfuko wa Shule za Kiislām (*Islamia Schools' Trust*) ambao ukaja kusaidia uanzishaji wa shule ya msingi ya kiislamu pale London mwaka unaofatia na shule ya sekondari baadae mwakani.

Yusuf Islam alijulikana zaidi kwa kuunga mkono kiuwazi kabisa hukumu ya kuuawa iliyotolewa na Ayatollah Khomeini kwa Salman Rushdie mnamo Februari 1989. "Salamin Rushdie, na waandishi wengine wote ambao wanamtusi Mtume Muhammad au Mtumemwengine yeyote, katika sheria za kiislām anatakiwa kuuawa," alisema hayo wakati ule wale wanaomtukana Mungu na dini



yake walipokuwa wanatafutwa. Akionesha kumtusi Mungu ni dhambi kubwa sana, alisema; “Kama ukimuuliza mwanafunzi yeyote wa Biblia akupe adhabu ya mtu kama huyu anayemtukana Bwana Mungu atakuwa hajatenda haki kama hatataja Mambo ya Walawi 24:16, “**Na yeye atakayelikufuru jina la Bwana hakika atauawa; mkutano wote watamwua kwa kumpiga kwa mawe; kama ni mgeni, kama ni mzalia, hapo atakapolikufuru jina la Bwana atauawa.**”

Yusuf Islam ameshatunukiwa tuzo nyingi mpaka sasa ikiwemo ya Tuzo ya Mtu wa Amani (*Man for Peace Award*) itolewayo na Mikhail Gorbachev kwa juhudi zake za kutangaza amani duniani, suluhishi baina ya watu na kuuondoa ugaidi; Mwaka wa 2005, alipata Udokta wa Heshima (*Honorary Doctorate*) katika Chuo Kikuu cha Gloucestershire kwa huduma zake katika elimu na ubinaadamu; 2007, *The Mediterranean Prize for Peace (Tuzo ya Amani ya Mediterranean)* huko Naples, Italia; Udokta mwengine wa Heshima kutoka Chuo Kikuu cha Exeter (10 Julai 2007), kwa huduma zake za kijamii na kusaidia kuongeza maelewano baina ya Waislamu na Wamagharibi.



Yusuf na Prince Charles ambaye alikiri kuwa alikuwa anapenda kusikiliza nyimbo za Cat Stevens.



Yusuf Islam na Tony Blair

Kwa sasa anaishi na mkewe Fauzia Mubarak Ali, na watoto wao watano huko Brondesbury Park, London na kutumia sehemu ya kila mwaka Dubai. Katika kuwajibu wale wanaotumia ubaya wa waislamu kupoteza ukweli wa Uislamu wenyewe, Yusuf Islam alisema:

“Itakuwa ni makosa kuuhukumu Uislamu kwa kutumia tabia za Waislamu waovu ambao wanatokezwa katika vyombo vya habari siku hadi siku. Ni kama kuhukumu gari iliyo nzuri kisa ndani yake kuna dereva mbaya ambaye kalewa na kuligongesha ukutani gari hilo. Uislamu unawaongoza binaadamu katika maisha yao ya kila siku- kiroho, kiakili na kimwili. Yatupasa tutazame vyanzo vya mafundisho yake kama Qur’an na sunnah za Mtume, hapo ndio tutaona ukweli wa Uislamu.”



**“Itakuwa ni makosa
kuuhukumu Uislamu kwa kutumia
tabia za Waislamu waovu ambao wana-
tokezwa katika vyombo vya habari siku
hadi siku. Ni kama kuhukumu gari iliyo
nzuri kisa ndani yake kuna dereva
mbaya ambaye kalewa na kuligo-
ngesha ukutani gari hilo.**





Njia ya Mawasiliano:

Tovuti: www.mountainoflight.co.uk
www.yusufislam.com
www.yusufislam.org.uk.

Anuani: 2 Digswell Street,
 London N7 8JX,
 United Kingdom.





[Islam, Yusuf. "My Journey from Cat Stevens to Yusuf Islam." Mountain of Light, 2001; Islam, Yusuf. "Questions for Yusuf Islam." By Deborah Solomon. The New York Times 7 Jan. 2007; Craig R. Whitney. "Cat Stevens Gives Support To Call for Death of Rushdie." The New York Times May 22, 1989; Brown, George. Cat Stevens: The Complete Illustrated Biography & Discography. George Brown, 2006; Islam, Yusuf. "Yusuf Islam." an interview by Nigel Williamson. Billboard magazine 25 Nov. 2006; Paphides, Pete. "Notions of Islam." The Times 6 July 2007; "Cat Stevens-one man, two identities." The Sydney Morning Herald 24 Sept. 2004; Schwartz, Stephen. "Why Yusuf Islam was turned away from the United States." The Weekly Standard. 22 Sept. 2004; "Cat Stevens becomes Yusuf Islam." video.google.com 16 Feb 2006. <<http://video.google.com/videoplay?docid=6157965900354777626>>; "Prince goes pop to praise school." bbc.co.uk 10 May, 2000. <http://news.bbc.co.uk/2/hi/uk_news/743894.stm>]

Jemima Goldsmith

“Uamuzi wangu wa kuingia katika Uislamu ulitokana na mimi mwenyewe”

~ Jemima Marcelle Goldsmith



Jemima alizaliwa London 30 Januari 1974 kutoka kwa bilionea wa Kiingereza Sir James Goldsmith na bibi Annabel Vane Tempest Stewart.

Alipitia Fransic Holland School Clarence Gate na Chuo kikuu Bristol. Akachukua shahada yale ya pili akisomea masomo yahasuyo Mashariki ya kati pale Chuo Kikuu cha London kitengo kinachosomesha masomo yahasuyo Afrika na Asia.

Amelelewa kama Mkristo wa Kiprotestant lakini akabadili dini kuwa Muislamu na kuchukua jina la Haiqa. Mrembo huyu Jemima, rafiki wa karibu sana na hayati Diana (Princess Diana), akaolewa na Imran Khan mwaka 1995; mchezaji kriket wa kipakistani aliyesoma Oxford. Katika kichwa cha habari *Why I Chose Islam* (*Kwanini Nilichagua Uislamu*), kilichowekwa na gazeti la *The Sunday Telegraph*, 28 Mei 1995, Jemima alisema:

“Nimechimba mwenyewe kwa kina vyote Qur’an na kazi za wanazuoni wa kiislamu mbali mbali..., hivyo kunipa muda wa kutosha kutafakari kabla sijafanya uamuzi huu. Kile kilichozanza kama upenzi wa kujua vitu kulistawi na kuchomoza kama ufahamu wa ukweli wa milele nao ni huu Uislamu.”

Na baadhi ya vilivyomvutia vikamfanya aamue kubadili dini ni maandiko ya Muhammad Asad, Gai Eaton, na Alija Izetbegovic.

**"Nimechimba
mwenyewe kwa kina vyote
Qur'an na kazi za wanazuoni
wa Kiislamu mbali
mbali"**

Jemima na mmewe walienda kuishi Lahore, Pakistan. Na mwaka 1997, Suleiman mtoto wao wa kwanza alizaliwa na bila kupoteza muda, Qasim mtoto wao wa pili alizaliwa miaka miwili baadae. Kama mjeruhiwa wa kutangazwa vibaya Uislamu katika vyombo vya habari, Jemima aliona

haja ya kuyasema haya:

"Kinyume na watu wadhaniavyo, uamuzi wangu wa kuingia katika Uislamu uliathiriwa na mimi mwenyewe, lilikuwa ni chaguo langu na wala sikufanya pupa...nimeelezea kina- gaubaga kuwa nimebadili dini kuwa Muislamu kutokana na upekuzi na maamuzi yangu mwenyewe. Jambo hili limed- harauliwa na vyombo vya habari. Pointi ya msingi nayotaka watu waiweke kichwani mwao ni kuwa, kubadili kwangu dini huku, hakuhusiani na ndoa kama wengi wadhanivyo. Naru- dia tena ilikuwa ni chaguo langu mwenyewe. Kidini, hakuna katakata kulazimishana kuingia katika dini kisa kwa ajili ya kuoana. Kama ielezavyo kwa uwazi yenyewe Qur'an kuwa, mwanamume wa Kiislamu anaruhusiwa kuoa watu wa kitabu (*Ahlul-Kitaab*) - kwa maneno mengine cidha Mkristo au Ya- hudi. Hata Sunnah ambayo ndio huelezea maisha ya Mtume mwenyewe inaonesha mjumbe wa Mungu alioa wote Mkristo na Myahudi.."

Jemima akawa balozi wa UK kwa UNICEF (Shirika la Umoja wa Mataifa Linashughulika na Watoto) mwezi Septemba 2001 na amekuwa akizunguuka Kenya, Afghanistan na Pakistan kwa shughuli hiyo. Amesaidia kuinua ufahamu kuhusu ilani za UNICEF ya kunyonyesha mtoto na kampeni za kutokomeza

unyanyasaji wa watoto ikiwa pamoja na ushirikishwaji wa watoto katika madawa ya kulevywa kwa namna moja au nyengine na watoto wadogo kufanyishwa kazi.



Jemima Goldsmith with her sons Suleiman and Qasim. Top right Picture, Jemima (left) with Princess Diana at Imran's cancer hospital in 1996

Akichangia kuhusu maisha, anasema:

“Imconekana furaha mwanamke wa Kimagharibi inategemea na uhuru wake kwenda klabu za usiku, kutumia vilevi na kuvua nguo; na kukosekana kwa uhuru huo katika jamii za kiislamu inaonekana kama kubanwa mwanamke katika haki zake za msingi, hata hivyo, kama tujuavyo wote, upuuzi huo unachangia kidogo sana katika furaha ya kweli...”



[Khan, Jemima. “Why I chose Islam.” The Sunday Telegraph 28 May 1995; “Imran and Jemima married in Paris.” The Times 17 May 1995; Khan, Sairah Irshad. “Jemima Khan.” Newsline 2002; “You ask the questions: Jemima Khan.” The Independent 28 Nov. 2001; “Imran Khan and Jemima divorce.” BBC News 22 June. 2004.]


Malcolm X

“Moja ya vitu ambavyo ningependa vijana wajifunze siku hizi, ni kuona wewe mwenyewe, kusikiliza wewe mwenyewe, na kufikiri wewe mwenyewe. Na hapo ndio utaweza kuja katika uamuzi wa busara kwa ajili yako wewe mwenyewe.”

~ Malcolm X akiongea na vijana wapigania haki zao huko Mississippi (1965).

“Hata wale wamchukiao wanaelewa uerevu wa akili zake- sio wa kawaida, hantabiriki na wa ki pekee...”

~ Oni kuhusu Malcolm X katika gazeti la *The New York*.



Malcolm X alizaliwa kama Malcolm Little Mei 19, 1925 huko Omaha, Nebraska. Baba yake, Earl Little alikuwa mchungaji asiyeogopa kusema ukweli, na pia alikuwa msaada mkubwa sana wa kiongozi wa Harakati za Weusi (Black Nationalist) wakati huo, Marcus Garvey. Malcolm X alilelewa katika imani ya kisabato na mama yake.

Maisha ya Malcolm mwanzoni yalikumbwa na masaiibu mengi. Kwa mfano, mwaka 1929 nyumba yao iliyopo Lansing, Michigan ilichomwa moto na kundi la wazungu lenye chuki;

alikuwa na umri wa miaka sita tu wakati baba yake alipokufa katika kifo kibaya sana; mama yake akawekwa katika hospitali ya

watu wenye matatizo ya akili (mtindio wa ubongo); akachukuliwa kwenda kulelewa katika vituo vya kulelea watoto wasio na uwezo; mwalimu wake alivunja ndoto zake za kuwa mwanasheria, alimwambia kazi hiyo haiendani na maniga (weusi), akamuusia awe fundi seremala akimsisitiza hata Yesu alikuwa seremala. Akaacha shule japokuwa alionesha ana uwezo mkubwa wa akili; akatumia sasa muda wake mwingi Boston, Massachusetts kufanya kazi za ajabu ajabu; japokuwa kazi yake ya mwanzo ilikuwa kung'arisha viatu; akasafiri kuhamia Harlem, New York ambapo akafanya uhalifu sana; kabla ya mwaka 1942, alikuwa mwongozaji vikundi vya madawa ya kulevya, umalaya, ukahaba, na kamari; na ilipofika mwaka 1946, alihukumiwa kwenda jela kwa miaka 10 kutokana na kukutwa na kosa la ujambazi (wizi wa kuvunja nyumba).

Malcolm X alijiongezea elimu yake wakati yuko jela. Ilikuwa humo humo gerezani ndio ambapo aliimeza *Dictionary* (alihiifadhi kichwani kamusi ya kiingereza yote), alisoma Biblia na kila kitu kuanzia somo linalohusu mabaki ya kale (Archeology) mpaka Somo la Uzazi na Kurithiana (Genetics). Wakati yupo humo gerezani, Malcolm akafata imani ya muislam mweusi na baada ya kuachiwa kutoka gerezani, akawa mjumbe katika Chama cha Waislamu Weusi (Nation of Islam) na kuchaguliwa kuwa msemaji wao. *Nation of Islam* ni kundi lilopotoka linalojinasibisha na Uislamu. Alijitoa toka katika Nation of Islam mwaka 1964 na kuanzisha kengine kiitwacho *Muslim Mosque, Inc* na pia akaunda *Chama cha Umoja wa Wamerika Weusi (Organization of Afro-American Unity)*, kundi ambalo linatetea uzalendo wa watu weusi. Baadhi ya Waislamu wa Kisunni walimuusia sana Malcolm kuusoma Uislamu wa kweli. Malcolm X alikubali ushauri ule ambao ukamfanya ajiengue kutoka katika Nation of Islam na baadae kukiri:

“Katika chuo kimoja na kengine ambapo nilipita kuongea katika mikutano isiyo rasmi, wengi kati ya watu weupe wamekuwa wakinfata wakijitambulisha kama waarabu, waMshariki-ya-Kati, au wanatoka kaskazini mwa Afrika na wapo hapa kimasomo, kikazi au wengine wana makazi ya kudumu. Wakawa wananiambia pamoja na maneno yangu ya kuwa-

chukia wazungu, ni kweli sikosei ninavyojichukulia kuwa ni Muislamu lakini walihisi niusome vizuri Uislamu, nitauelewa na kuukubali. Kama mfuasi wa Elijah (kiongozi wa Nation of Islam), nilikasarishwa na walichokuwa wakinisema. Lakini baada ya hali hii kujirudia kwa muda, nikajiuliza mwenyewe, kama kweli mtu yuko kidhati katika kuitangaza na kuifata dini hii, iweje mtu arudi nyuma katika kujiongezea maarifa ya kuijua dini hiyo zaidi na zaidi?!”

Mmoja wa hao Waislamu waliojitolea alikuwa Dkt. Mahmoud Youssef Shawarbi ambae nae aliongozwa na kauli ya Mtume “Mmoja wenu hawezi kuamini mpaka ampendelee mwenzake kile akipendacho nafsini mwake.”⁴⁹ alimshauri Malcolm kuukubali uislam wa kweli. Baadae Malcolm alifunga safari kwenda kuhiji Makkah ambapo aliugundua uislam wa ukweli na akawa muislam wa Kisunni akatoa shahada upya (mwenyewe) na kubadili jina lake kuwa Al-Hajji Malik Al-Shabbazz. Malcolm alikuwa na furaha baada ya kukamilisha Hijja yake akisema amefurahi kuwa mweusi wa kwanza kwa wazaliwa wa Marekani kuhiji. Siku zake za kuhiji zilileta mabadiliko kuhusu msimamo wake wa kuchukia weupe. Akasema:




**“Mimi ni Muislamu
na nitaendelea kuwa
hivyo. Dini yangu
ni Uislamu.”**

“Kulikuwa na makumi elfu mengi ya mahujaji kutoka sehemu mbalimbali duniani, walikuwa watu wa rangi zote, kuanzia wale wazungu wenye macho ya rangi ya samawi mpaka Waafrika Weusi. Lakini wote tulikuwa tukishiriki katika ibada kuonesha imani ya mshikamano na umoja ambayo katika maisha yangu ya Marekani siku-

wahi kuota kuwa itawezekana...Amerika inapasa kuufahamu uislam, kwa sababu hii ndio dini iliyoondoa tatizo la ubaguzi wa rangi katika jamii wakati dini hii iliposhushwa. Katika ku-

49. Bukhari Vol. 1, Bk. 2, No. 12.

zunguuka kwangu katika mataifa ya Waislamu nimekutana, nimeongea na hata kula pamoja na watu ambao Marekani walikuwa wakichukuliwa ni weupe (wazungu).- lakini kwa hawa ile tabia chafu ya kibaguzi ya uweupe imeondoshwa katika fikra zao kwa Uislamu wao. Sijawahi kuona kabla, upendo huu wa dhati ambao hawa wanautekeleza bila kuzingatia tofauti zao za rangi.”



Wakati akiwa Hijja, aliandika barua kwa wasaidizi wake wa chama chake kipya (*Muslim Mosque*) kule Harlem na kuwaomba wazisambaze kwenye vyombo vya habari. Aliandika:

“Sijawahi kushuhudia ukarimu mkubwa na roho ya udugu wa kweli kama niliouona ule wa rangi zote kule ardhi takatifu, nyumba ya Ibrahim, Muhammad na mitume wote waliopita. Kwa wiki nzima sikuwa mzungumzaji ila ni kushangazwa tu kwa yale mapenzi yalioneshwa kwangu na wale watu wenye rangi tofauti....najua mnaweza kushangazwa na maneno haya yanayotoka kinywani mwangu. Ukweli hijja hii, imenilazimisha kubadili fikra zangu ambazo zilikuwa zimejaa mwanzoni na sasa nimeamua kutumia upande mwingine wa shilingi kwa baadhi ya mambo niliyokuwa nayaamini. Hili halijakuwa gumu kwangu. Japokuwa nimekuwa nikiiamini imani yangu kidhati, siku zote nimekuwa mtu mwenye kujaribu kukumbana na ukweli, na kuukubali uhalisia wa maisha. Siku zote nimekuwa ni mwenye kukiwacha kichwa changu wazi ili kiweze kwenenda mkono kwa mkono na utafutaji mzuri wa ukweli. Katika kipindi cha siku hizi kumi na moja zilizopita, nimekula chakula kutoka katika sinia moja, nimekunywa kwa kutumia bilauri moja, na nimelala katika sehemu moja –huku tukiabudu kuelekea kwa Mungu mmoja- pamoja na Waislamu wenzangu, ambao macho yao ni ya rangi ya kisamawati kuliko! Wenye nywele zenye umanjano kuliko! Na wenye ngozi yenye weupe pe! Ila kwa maneno na matendo ya Waislamu hawa weupe, nimeji-hisi kama niko pamoja na wenzangu (Waislamu weusi) kutoka Nigeria, Sudan na Ghana. Kwa kweli kila mtu alikuwa kaka wa kweli kwa mwenzake, kwani ile imani ya kuabudia Mungu mmoja imeondoa kule kujiona kutoka vichwani mwao, kutoka tabia zao na hata kutoka katika hulka zao. Nimeona kweli kama wazungu wa Marekani wangekubali kuabudia Mungu mmoja basi bila shaka wangekubali umoja wa binadamu pia kuepuka kuwadhuru wenzao kwa sababu ya tofauti rangi tu. Kwa ubaguzi huu unaoenea Marekani kama saratani isiyo na tiba, tulitegemea wale wazungu wanaojiita wana mioyo ya kristo basi wangelivalia njuga tatizo hili kwa kufanya harakati za kulito-

comeza. Huu ndio ulitakiwa uwe muda mahsusi wa kuiokoa Marekani kutokana na janga hili kubwa – janga lililoimaliza Ujerumani baada ya kuwamaliza Wajerumani wenyewe. Waliponiuliza kuhusu lipi lililokuvutia katika Hijja nikajibu ni huu udugu wa kweli, watu aina tofauti, wenye rangi tafauti, tokea maeneo tofuati duniani wanakuja kukaa pamoja na kuwa kitu kimoja! Kwa kweli jambo hili limenionesha nguvu za Upekee (U-moja) wa Mungu. Wote tumekuwa tukila kimoja, tukilala sehemu moja, kila kitu tulikifanya kwa pamoja katika kumuelekea Mungu mmoja.”



Malcolm X akiwa na Mfalme Faisal wa Saudi Arabia, Julai 1964.

Malcolm X akarudi kutoka Hijja akiwa mtu tofauti, akiwa yuko katika silika yake ya asili kama alivyo mtoto asiye na dhambi hata kidogo, kabla ya kubadilishwa na mazingira. Mtume wa uislam, Muhammad alisema, “**Yule anayekuja kwenye nyumba ya Mungu (Kaa’ba) akiwa na niya ya kuhiji na asiwe mwenye kusema au kutenda ovu, basi atarudi akiwa kama mtoto aliyetoka kwa mama**

yake punde.”⁵⁰. Kutokana na hivyo, kule kuchukia weupe kwa Malcolm-X kulisafishwa baada ya kujifunza Uislamu huu wa kweli. Na tarehe 27 Disemba 1964, Malcolm alisema, “Nadhani hii ndiyo sababu kwanini Uislamu unaenea siku hadi siku. Uislamu hauna ubaguzi wa rangi hata kidogo katika mafundisho yake. Hakuna mafundisho yanayokutaka umhukumu mtu kwa rangi yake. Hata uwe na rangi gani katika Uislamu, utabaki kuwa Muislamu na utabaki kuwa ndugu yetu.”




Malcolm X akiwa na Fidel Castro, Octoba 1960.

50. Muslim Bk. 7, No. 3129. Na pia katika Bukhari Vol. 2, Bk. 26, No. 596, Mtume Muhammad anasema, “Yeyote atakayetekeleza Hajj kwa nia ya kutaka radhi za Allah, na asifanye tendo la jima’a na mke wake, na asifanye maovu au madhambi, basi atarudi (kutoka Hajj akiwa hana dhambi lolote) kama kwamba amezaliwa upya.”



Malcolm alibahatika kutembelea maeneo tofauti tofauti ulimwenguni na kukutana na watu mbali mbali wenye haiba kubwa. Miongoni mwa nchi alizotembelea ilikuwa ni Saudia Arabia ambapo alikutana na Muhammad Faisal; mjukuu wa mfalme; Ghana ambapo alikutana na Kwame Nkrumah, Misri ambapo alikutana na Gamal Abdel Nasser; Aljeria na kukutana na Ahmed Ben Bella, kiongozi mkuu wa mapambano ya Aljeria



Malcolm X akiwa na Adbulrahman Muhammad Babu ambaye alikuwa mwanasiasa, msomi na kiongozi wa mapinduzi na ashawahi kuwa waziri katika serikali ya Tanzania.

dhidi ya wakoloni Wafaransa, na alikuwa waziri mkuu wa mwanzo wa Aljeria (1962-63) na akawa rais wa kwanza (1963-65). Pia, Malcolm alitembelea Nigeria ambapo akafanya muhadhara mkubwa chuo kikuu Ibadan. Nchi nyengine ni Ethiopia, Tanzania, Guinea, Sudan, Senegal, Ufaransa, Liberia na Morocco. 21 Sept 1960, Malcolm alikutana na Fidel Castro katika hoteli ya Theresa, Harlem. Tarehe 3 Disemba mwaka wa 1964, Malcolm alikuwa Uingereza akishiriki mdahalo, Oxford. Yeye akawa upande wa

kutetea kichwa cha mdahalo kilichobeba ujumbe “*Siasa Kali (isiyo na kadiri) Katika Kuntafuta Uhuru Sio Kosa, na Siasa Poa (mwendo wa kiasi) Katika Kutafuta Haki Siyo nzuri.*” Kwa Kiingereza kichwa cha mdahalo ni “*Extremism in the Defense of Liberty is No Vice; Moderation in the Pursuit of Justice is No Virtue*” Na mdahalo huo ulirushwa na televisheni kwa taifa zima na BBC. Katika mdahalo, Malcolm X alijitamba kwa fakhari kabisa, “Uislamu ni dini yangu, namuamini Allah, na namuamini Muhammad.”

Akiwa anafanya muhadhara katika ukumbi wa Manhattan 21 Februari 1965, washika mitutu watatu walimsogelea Malcolm karibu na jukwaa na kummiminia risasi 15. Malcolm akiwa na miaka 39, alitangazwa ameshaaga dunia mara tu mwili wake ulipowasili katika hospitali ya kidini ya Columbia, New York. Akazikwa katika makaburi ya Ferncliff huko Hartsdale, New York. Ossie Davis (1917-2005), mwigizaji na mwongozaji filamu wa kimarekani, mshairi, mwandishi na mpiganaji wa haki za binaadam, alitoa hotuba katika msiba huo wa Malcolm X, aliyeipa kichwa “*Mwanamfalme Mweusi Aliyeng’ad*”:

“Kuna wale watakaotufunza kumchukia na kutomkumbuka. Watakaotufunza kujinusuru kwa kutomuandika katika zamu zetu hizi. Wengine watauliza ni lepi mnalojivunia kwa kiumbe huyu mwenye hasira, mtukutu, mtata, na jeuri – na sisi tutamuangalia tukitabasamu. Wengine watasema – jiupusheni naye kwani hakuwa binaadamu bali ni shetani, katili, mchochezi maovu na adui wa watu weusi – pia na huyu tutamuangalia na kutabasamu. Watamwita mbaguzi, mwenye chuki, mtu ambaye ataharibu tu katika harakati zenu za kujikwamua! Tutajibu kwa kusema: Walishawahi kuongea kweli na Malcolm? Walishawahi kumgusa? Walishawahi kumsogelea na kupata tabasamu lake? Hivi walimsikiliza kidhati kweli? Alishawahi kufanya hayo mnayomzulia? Je kweli kashawahi fanya lolote lenye hila? Na je ni kweli alijihusiha na ugomvi au vurugu zozote? Kwa maana kama hukumjua basi na umjue. Na kama ungemjua basi ungeelewa kwanini tunamkumbuka na kumuheshimu.”

Dkt. Martin King wa pili, alishtushwa na taarifa za kifo chake. Martin aliandika:

“Hatukuiona njia ya jicho kwa jicho kama njia ya kuondoa tatizo la ubaguzi wa rangi, lakini siku zote nimekuwa ni-kimuona Malcolm kama mtu mwenye uwezo mkubwa wa kuweka kidole chake pale kwenye mzizi wa tatizo. Alikuwa ni mzungumzaji mzuri sana kwa yale aliyoaamini, na hakuna atakayediriki kukataa kuwa Malcolm alikuwa akiumizwa sana na matatizo ya rangi yaliyokuwa yakitupata.”

Vyombo vya habari kutoka mataifa mbalimbali yalijawa na simanzi nzito kwa kuondokewa na mtetezi na mwanaharakti huyu mkubwa mwenye asili ya Afrika katika historia ya Marekani. Mathalan, *The Daily News of Lagos*, Nigeria liliandika, “Malcolm X alijitolea na kuwa na msimamo katika harakati za kujikwamua na ubaguzi kwa ajili ya ndugu zake na hakuna anayepinga hilo... alipigania na kufa kwa kile alichokiamini. Bila shaka atapata nafasi yake katika jumba kubwa la mashahidi.”

Waislamu hawaoni kauli yenye kumpa heshima Malcolm x kuliko aya hii ya Qur'an:

“Wala msiseme kuwa wale walio uwawa katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni maiti; bali hao ni wahai, lakini nyinyi hamtambui.”

[Q 2:154].

Marekani, picha ya Malcolm imekuwa ikitumika katika stempu za posta. Na shule nyingi, mitaa, na barabara zimekuwa zikipewa jina lake kwa ajili ya kumkumbuka. Baadhi ya vyuo na shule hizo ni *Malcolm X Community College* huko Chicago, *Malcolm X Liberation University* pia Durham, N.C, *The Malcolm X Society*, *Malcolm X Shabazz High School* iliyoopo Newark, New Jersey, *Malcolm Shabazz City High School* nayo iliyoopo Madison, Wisconsin; mtaa wa Reid uliopo Brooklyn, New York ulibadilishwa na kuwa *Malcolm X Boulevard*; mwaka 2005 chuo kikuu Columbia kilitangaza ufunguzi



wa kituo cha elimu walichokiita *Malcolm X and Dr. Betty Shabazz Memorial and Educational Center*. Afrika ndio kawaida kabisa kuona mabasi yameandikwa Malcolm X au watu wamevaa fulana zenye picha yake. Hayo yote tisa, kumi; Malcolm X alijitolea kusambaza uislamu sio tu Marekani bali kwa wote dunia nzima. Kutoka kwake katika kundi lililopotoka la *Nation of Islam* na kuingia katika Uislamu sahihi kuliacha athari hadi kwa mtoto wa Elijah Muhammad, Wallace Muhammad ambae baada ya kifo cha baba yake alikiongoza chama cha *Nation of Islam* kufata yale aliyofanya Malcom kwa kufata Uislamu sahihi. Na kwa kweli, kitabu cha historia yake “*The Autobiography of Malcolm X*” kimewafanya wengi waingie katika Uislamu.

Malcolm x alioana na Betty X (aliyezaliwa kama Betty Sanders) maeneo ya Lansing, Michigan mwaka 1958. Walikuwa na watoto wa kike sita, Atallah Shabazz aliyezaliwa Novemba 1958, Qubilah Shabazz (Disemba 1960), Ilyasah Shabazz (Julai 1962); Gamillah Shabazz (Julai 1964) na mapacha Malaak na Malikah Shabazz waliozaliwa baada ya kifo chake Septemba 1965.

Mwanahistoria Robin D.G Kelley aliandika:

“Malcolm X kashaitwa majina mengi: mwanaharakati wa weusi, baba wa taifa la weusi, mdini, msiri, mjamaa, na kitisho kwa jamii. Maisha yake – siasa na itikadi zake – yanakubaliwa kwa



sehemu ndogo... Malcolm amekuwa mfano wa mtihani wenye machaguo huru ambapo kila mtu anaweza kuandika alivyoelewa yeye kuhusu siasa na itikadi zake. Chuck D kutoka kundi la Rap litwalo *Public Enemy* na Jaji wa mahakama Clarence Thomas wote wanamwita Malcolm X kama shujaa wao.”

Baadhi ya Dondoo Zake Mashuhuri

“Mtu asiyesimamia chochote basi ataanguka kwa chochote.”

□□□

“Hakuna atakayekupa uhuru, hakuna atakayekupa usawa na haki, kama wewe ni mwanaume nenda uichukue.”

□□□

“Sababu za wazayuni kubalalisha uwamizi wa Izrael katika ardhi ya Palestina hazina mashiko ya kiakili wala kihistoria.”

□□□

“Hautakini uwe kipofu kwa uzalendo wa nchi yako mpaka unashindwa kupigania ukweli. Baya ni baya tu, haijalishi live linemafanywa na nani au kusemwa na nani.”

□□□

“Shule yangu ilikuwa vitabu na maktaba nzuri... nilitumia maisha yangu yote kule nikiwa nasoma, nikitimiza azma yangu ya udadisi.”

□□□

“Elimu ni pasipoti yetu ya baadae, kwani kesho iko kwa ajili ya wanaojitayarisha nayo leo.”

□□□

“Tangu nikiwa mdogo nilijifunza kama unahitaji jambo basi fanya kekele.”

□□□

“batuwi na fujo kwa mtu ambaye batufanyii fujo.”

□□□

“Dhumuni letu ni kuwa na uhuru kamili, usawa na haki kwa njia yoyote ile itakayohitajika.”

□□□

“Ukweli upo katika upande unaoonewa”

□□□

“Huwezi kutenganisha amani na uhuru wa kweli, kwa maana hakuna atakayekuma na amani kama hana uhuru.”

□□□

“Hutakwini kuwa mtu tu, eti ili upigane baki yako, unachotakwina kufanya ni kuwa mtu mwerevu, mjanja.”

□□□

“Kama hautakuwa tayari kufa kwa ajili yake, basi liondoe neno ‘uburu’ katika kamusi yako”

□□□

“Gharama ya uhuru ni kifo.”

□□□

“Mimi ni yule mtu niliye kama wewe unavyofikiri ulivyo...Ukitaka kujua nitakufanya nini, jaribu kufikiria ingekuwa wewe ungefanya nini. Nitafanya hilo hilo kwako tena nitaongeza kidogo.”

□□□

“Hata iwe heshima ya ukubwa gani wanayoionesha kwangu mimi, hata uwe utambuzi gani wanaotumia hawa wazungu kutambua uwepo wangu mimi, ili mradi bado heshima hiyo haioneshwi kwa kila mmoja wetu bado siooni na sübitaji heshima hiyo kwangu.”

□□□

“Haimaanishi kuwa nahamasisha utumizi wa nguvu na vurugu, lakini pia sipingi kutumia njia hii kwa ajili ya kujilinda. Siiti njia hii ni ya vurugu tunapoongelea kisasi bali naiita ukuaji wa akili.”

□□□

“Utamshukuru vipi mtu kwa kukupa kitu ambacho tayari chako? Na cha kushangaza ni pale unapawaona watu wakishukuru kupewa sehemu tu ya kile ambacho tayari ni chao.”

□□□

“Ni muda wa kufa shabidi sasa, na kama ikatokea kuwa miongoni mwao, basi itakuwa kwa ajili ya udugu wetu. Na hilo ndilo jambo pekee litakaloweza kuokoa taifa hili.”

□□□

“Haiwezekani ubepari uendeleo kwepo, kimsingi huu mfumo wa ubepari unabitaji damu ya kunywa. Ubepari ulikuwa kama tai, lakini sasa umeshakwaa kindi lake. Ulikuwa na nguvu ya kunyonya damu ya yeyote bila kujali unanguvu au la. Lakini sasa umekuwa mfumo wakioga, ukinyonya damu ya wasiojiweza tu. Kwa uhuru huu, unaowafikia mataifa mbalimbali, ubepari umekuwa ukijeruhi wachache, unanyonya damu ya wachache, na unakuwa dhaifu kila siku. Naimani kwa kipindi kifupi, utamalizika kabisa.”

□□□

“Mfumo mpya wa maisha uko njiani kuja, ni jukumu letu kujitayarisha ili tuchukue sebemu zetu, tulizo na baki nazo katika maisha hayo.”

□□□

“Mimi ni mfuasi wa ukweli, bila kujali nani kausema. Natetea baki, bila kujali nani anapinga au nani anatetea. Mimi ni mwanadamu, na naunga mkono yeyote au chochote kitakacho mfaidisha mwanadamu.”

□□□

“Naamini dini inayoamini uburu. Kwa dini yoyote ambayo haitanirubusu nipigane kwa ajili ya kutetea watu wangu, bora na iende tu dini hiyo.”

□□□

“Mimi ni Muislamu, kwa sababu ndiyo dini inayofundisha jicho kwa jicho na jino kwa jino. Inakufundisha kubeshimu kila mtu, na kujali baki za wote. Lakini pia inafundisha iwapo mtu akitokea akakukanyaga kwa kukuonea, kata miguu yake. Nitabeba shoka la dini yangu kila mahali.”

□□□

“Hakuna mafundisho katika kitabu chetu yanayotugiza tuumie kimya kimya. Dini yetu inatufundisha tuwe waerevu. Kuwa mtu wa amani, kuwa na huruma, tii sheria, na umubeshimu kila mtu; lakini akitokea mtu na kunyanyua mkono wake kwako usisite kumpeleka kaburini.”

□□□

“Mimi ni Muislamu na nitaendelea kuwa hivyo. Dini yangu ni Uislamu.”

□□□

“Sio tu Marekani ndio wanaotakiwa kufahamu na kuuelewa Uislamu bali ni watu wa dunia nzima.”

□□□

“Kwa kila umuonapo mtu anafanikiwa kuliko wewe, huwa anafanya jambo ambalo wewe hulifanyi.”

□□□

“Kukaa tu mezani hakukupi chakula. Unatakiwa ukile kile kilichokuwa katika sabani. Kuwa hapa Marekani hakukufanyi wewe uwe mmarekani. Kuzaliwa hapa marekani hakukufanyi pia uwe mmarekani.”

□□□

“Kama nikifa huku nikifanikisha kuileta nuru yoyote, nikiwa nimesambaza ukweli wowote utakaosaidia kuua sumu ya saratani hii ya ubaguzi inayoshambulia mwili wa Marekani, basi shukrani zote zinamstabiki Allah na makosa yote yatabaki kuwa yangu.”

□□□

“...Kwa njia yoyote ile itakayohitajika”

□□□

“Sifa zote njema zinamstabiki Allah, Mola wa walimwengu wote.”

□□□



Pia inatupasa tuifikirie kwa makini hotuba ya kukumbukwa ya Malcolm itwayo *The Field Negro and The House Negro (Mwenzi wa Msituni au Mwenzi wa Nyumbani)*. Kwa sababu watu duniani (na tena watu wa rangi zote) huwa wanagawika katika makundi haya mawili. Na baada ya hotuba hii jiulize mwenyewe kama wewe ni Field Negro au ni House Negro! Na sasa naomba tumkaribishe kaka Malcolm X aweze kutunasihia:

“Kulikuwa na aina mbili za watumwa. Kulikuwa na yule wa nyumbani na mwingine anayezurura. Yule wa nyumbani alishi katika nyumba na bwana wake. Alivaa vizuri. Alikula vizuri pia kwani alikula kile kilichoachiwa na bwana wake. Akiwekwa darini au chini kabisa mwa nyumba (katika msingi), hata hivyo bado aliishi karibu na bwana wake. Waliwapenda wamiliki wao kuliko hata hao mabwana kujipenda wenyewe. Walidiriki kujitolea hata maisha yao ili kuulinda nyumba ya mmiliki wake. Tena kwa haraka kuliko hata huyo bwana mwenyewe. Kama tajiri wake akisema, “Tuna nyumba nzuri hapa” basi yule mningro atarukia, ‘Kweli bosi, tuna nyumba nzuri.’ Kila wakati ambapo bosi atatumia ‘sisi’ na yeye hatosita kutumia neno hilo. Hivyo ndivyo walivyokuwa.

Kama nyumba ya bosi ikashika moto, yule mtumwa atakimbia zaidi kuuzima moto kuliko hata mwenye nyumba mwenyewe. Kama bwana akiumwa, utamkuta mtumwa wake akiuliza, vipi bosi hata sisi tunaumwa (kwa hali ya kumsikitikia na kumliwaza bosi wake)!? Alijitahidi kumtambua bosi wake zaidi ya bwana wake kujitambua mwenyewe. Na hata ukienda kumtembelea mwenzako huyu ukimuasa mtoroke! Utakuta anakuangalia kwa jicho la mshangao na kusema, “He! Umewehuka!? Una maana gani unavyosema tutoroke!? Wapi nitakaa katika nyumba nzuri kama hii? Wapi ntavaa nguo nzuri kuliko hizi? Wapi ntakula chakula kizuri kuliko hiki?” Huyo ndiyo Nigro wa nyumbani. Kwa kipindi hiko, aliitwa ‘Niga’ wa nyumbani. Na hivyo ndivyo tuwaitavyo sasa, kwani bado tunao humu ndani wanazunguuka zunguuka kuturudisha nyuma mitaani.

Huyu Mnegro wa kisasa anampenda bosi wake sana. Anataka aishi karibu naye. Atadiriki kulipa mara tatu ya thamani ya nyumba ili apate nafasi ya kuishi karibu na mabosi wake (wazungu), na kutamba kwa wenzake, “Mimi ndio Mnegro pekee hapa. Ndio pekee katika kazi hii na ndio pekee katika shule hii.” Tunakwambia wewe sio chochote zaidi ya mtumwa wa nyumbani tu kama wale wanegro wa zamani. Na kama mwenzake akija kukushauri kuondoka hapa, unasema kile kile alichosema mnegro wa kale katika mashamba, “Unamaanisha nini ukisema tuondoke? Tutoke Marekani? Nchi hii nzuri ya wazungu? Sijasahau lolote Afrika.” Na wakati umeiacha akili yako Afrika.

Katika kipindi hiko hiko cha kilimo cha kutumia watumwa, kulikuwa na kundi la pili ambalo ni la Mnegro asiye na makazi kwa bosi wake. Hawa walikuwa wengi. Sema kweli hawa walikiona cha moto. Walikula yaliyosazwa ndani. Walikula vile vilivyoachwa na watu wale wachafu (nguruwe) ndani. Siku hizi mnaita Chit’lins (chakula kitokanacho na utumbo wa nguruwe). Zama hizo waliziita kama zilivyokuwa, matumbo! Na baadhi yenu bado ni walaji matumbo hayo hapa.

Mnegro huyu wa shambani alipigwa kuanzia asubuhi mpaka jioni. Aliishi bandani tu. Alivaa mitumba. Alimchukia bwana wake. Nasema alimchukia bwana wake na inaonyesha alikuwa na akili. Yule wa nyumbani alimpenda bwana wake huyu alimchukia, tena kwa kuwa walikuwa wengi, waliwachukia mabwana zao. Kama nyumba ya bosi wao ikishika moto, wala hutamkuta akiisumbua kuuzima moto ule, bali akijitenga kuomba dua upepo uzidi kuvuma na moto uongezeke. Kama bwana wa watumwa akiumwa, basi wataomba afe kabisa. Kama mtu akija kwa hawa na kuwaambia watoroke. Hawakuuliza tunaelekea wapi bali walihisi sehemu nyengine yoyote ni bora kuliko ya hapa. Tunao watumwa hawa Marekani ya sasa, na mimi ni miongoni mwao. Hatusikii siku hizi wanegro wakilalama eti, “Serikali yetu ina matatazo” bali wanasema “Serikali ina matatizo”. Nishawahi kumsikia mmoja akisema, “Wanaanga

wetu” na wakati hata haruhusiwi kusogelea maeneo hayo. Au mtu atumie “Jirani zetu, wanaanga wetu au wanamaji wetu” kwa hawa wazungu, bila shaka atakuwa kapotelewa na akili. Nasema huyu Mnegro atakuwa kapotelewa na akili.

Kwa kuwa bwana wa watumwa wa zama hizo alimtumia Tom kulinda wenzake, ndio hicho hicho kinachofanyika sasa kwani hawa vibaraka sio lolote zaidi ya kuwa ni wajomba Tom wa kisasa tu. Kina wajomba Tom wa karne ya 20 wanatumika kutulinda sisi na wanaturudisha nyuma. Wanatufanya tupende amani ambayo ni ya uongo. Tusiwe na vurugu. Huyu ni yule yule Tom anaekufanya uwe hivyo ili uendelee kutawaliwa. Ni sawa sawa umeenda kwa tabibu wa meno ambaye atakutoa jino lako, utampiga tu pale atapoanza kuvuta jino. Sasa itabidi akuweke vitu katika taya zako ili usikie ganzi, na hapo utakuwa unaumia kwa amani kabisa. Damu itakuwa inamwagika katika taya zako na wewe hatuahisi chochote kikiendelea. Eti kwa sababu kuna mtu amekufanya uumie kimya kimya! Hahaha!

Wazungu wanatufanyia jambo hilo hilo mitaani humu. Anapotaka kukufunga fundo kichwani mwako, kukutumia atakavyo na asiwe na hofu ya wewe kupigana naye, huwa wanawatumia hawa kina wajomba Tom, wanaojifanya viongozi wa dini kama ile ganzi ya kwenye meno, wakituelekeza tusiache kuumia ila tumie kimya kimya! Kama mchungaji Cleage alivyosema, wanatufundisha damu yetu imwagike mitaani. Hii ni aibu ukizingatia yeye ni mchungaji wa dini. Kama ni aibu kwake nadhani mnaelewa kwangu itamaanisha nini.

Hakuna kitu kama hicho katika kitabu chetu Qur'an kama nyie mnavyoiita Koran! kitufundishacho kuumia kwa amani. Dini yetu inatutaka tuwe na akili. kuwa na ustahifu (uungwana) lakini pia kuwa na amani ya kweli. Tii sheria. Mheshimu kila mtu. Lakini kama mtu akijaribu kunyanyua 'kamkono' chake kukudhuru, usisite kumpeleka kaburini. Hii ndio dini bora. Tena ndio ile ile dini ya zamani. Hii ndio dini mama na baba walikuwa wakiiota. Jicho kwa jicho, jino kwa jino, kichwa kwa

kichwa na (uhai) maisha kwa (uhai) maisha. Hii ndio dini bora. Na kwa yeyote anayepinga dini hii isifundishwe, ni mbwa mwitu anayetaka kukufanya chakula chake.

Hivi ndivyo ilivyo kwa wazungu hawa wa Marekani. Ni mbwa mwitu na wewe ni mbuzi. Muda ambao sijui mchungaji, au padri anakufundisha usimkimbie mzungu huyu na tena anakufundisha usimpige vita mzungu si jengine ila atakuwa mnafiq kwako na kwangu mimi. Uweke maisha yako rehani kiasi hicho?! La hasha, yalinde maishe yako, linda uhai wako. Ndio jambo lenye thamani zaidi kwako. Na hata kama ikatokea unahitaji kukata tamaa nayo basi jitahidi iwe mechi suluhu.

Mabwana hawa wa watumwa waliwachukua kina Tom, wakiwavalisha vizuri, wakiwalisha vizuri na hata kuwapa elimu kidogo. Waliwakabidhi makoti marefu na kofia nzuri juu na watumwa wengine wote wawatazame wao. Kisha ikawa rahisi kuwatawala wale waliobakia kupitia Tom. Nyenzo hiyo hiyo iliyotumika kipindi hicho ndiyo itumikayo leo. Anamchukua Mnegro mmoja na kumfanya mashuhuri, anamjenga, anamtangaza na kumfanya awe mzungumzaji na kiongozi wa wanegro.”



Malcolm X akiwa na Martin Luther King

Tovuti:


www.cmgww.com/historic/malcolm/

www.brothermalcolm.net/

www.malcolm-x.org/

[www.koranselskab.dk/profiler/](http://www.koranselskab.dk/profiler/malcolmx.htm)

malcolmx.htm



references

[Malcolm X. The Autobiography Of Malcolm X. New York: Grove Press, 1966; Clarke, John Henrik. Malcolm X: the Man and His Times. New York: Macmillan, 1969; Decaro, Louis A. On The Side of My People: A Religious Life of Malcolm X. New York: New York University, 1996; Carson, Clayborne. Malcolm X: The FBI File. New York: Carroll & Graf Publishers, 1991; Breitman, George. Malcolm X Speaks: Selected Speeches and Statements. New York: Grove Weidenfeld, 1990; Breitman, George (ed). Malcolm X: By Any Means Necessary. New York: Pathfinder Press, 1998; Rickford, Russell J. "Betty Shabazz, Surviving Malcolm X," Illinois: Sourcebooks, Inc., 2003; "Malcolm X." The New York Times 22 Feb. 1965; Joe Auciello "Malcolm's Advice to Young People: 'Think for yourself.'" Socialist Action 1 May 2005. v.23, n.5; The Autobiography of Malcolm X. Princeton, N.J.: Films for the Humanities & Sciences, 2001. (Video Tape, 53 min.); The Speeches of Malcolm X. Orland Park, IL: MPI Home Video, 1997. (Video Tape, 40 min.)]

Fidelma O'Leary



O'Leary, mzungu mwenye macho ya

kijani

wa N

Chuo

Austi

Kaso

katika

Healt

B.E.

Kiku

kuhoj

kwayo, na baadae kuamua kusoma
na mwishowe akabadili dini kuwa
akijiuliza kwa mshangao, "Kama
anamuabudia Mungu?" kutokan
familia ya
tena kwake.

Mwisho w

PRODUCT DESCRIPTION

Format: Paperback

Print Length: 672 pages

Author: Salim Boss

Publisher: Extremely Smart

Language: Kiswahili

ISBN: 978-9966-1628-1-6

Product Dimensions: 5 x 7.8 x

1.4 inches

Colour: Full colour on all pages

Weight: 0.9 kg

Price: Tshs. 17000 / Kshs 900 /

Others, \$ 11 US

UKITAKA KUNUNUA KITABU, TAFADHALI

"Uislamu ni mwendelezo wa imani ambayo nilikuwa nayo
mwanzo. Uislamu unafanana na kila kitu ambacho kinabadilisha na sasa
moyo wangu uko katika amani nikiwa na dini ya kale. Uislamu
galau ilinichukua safari ndafu iliyokuwa na mwanadamu." -

WASILIANA NA:

Tanzania +255 658 091 609 au +255 685 661 331
Kenya +254 720 641 541
Email extremely_smart@yahoo.com
Website www.muerevumno.wordpress.com

Dkt. Fidelma O'Leary
filamu iliyoenea sana ihusuyo hiya,